# KUCHUNGUZA FANI NA DHAMIRA YA MALEZI YA WATOTO KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO RIWAYA YA WATOTO WA MAMA N'TILIE

**ZAINA OMAR OTHMAN**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNIKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI - FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini, anathibitisha kuwa, amesoma tasnifu hii iitwayo **Kuchunguza Fani na Dhamira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano** ***Watoto wa Mama N'tilie*** na amependekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunikiwa Shahada ya Uzamili (M.A) katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

………………………………

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**Msimamizi**

**……………………………**

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielekroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyengine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

.

# TAMKO

Mimi, **Zaina Omar Othman,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyengine yoyote.

Sahihi………………………………

Tarehe……………………………….

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa Ami yangu Bw. Said Othman Khammas

# SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mola wangu (Subhallah Wataalah), kwa kunijaalia na kunipa afya, nguvu na uwezo wa kufanikisha utafiti huu na kwa kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati na upendo kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii Daktari, Mohamed Omary Maguo kwa kunifuatilia kwa ukaribu sana na kuniongoza vizuri hatua kwa hatua ya utafiti huu bila ya kuchoka na kusita hadi kuikamilisha. Aidha kutokana na juhudi zake hizo nina muombea kwa ALLAH (S.W) ampe umri mrefu wenye kheri nae ili azidi kuendelea kutoa taaluma kwa wote. Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengine wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunifundisha vizuri na kuniongoza katika muda na kipindi chote cha masomo yangu.Miongoni mwa walimu hao ni: Profesa E. Mbogo, Profesa T.S.Y.M. Sengo, Dkt. Lipembe, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Hilda Pembe, Dkt. Zelda Elisifa, Mw. Nassor Ali Suleiman na wengineo pamoja na mlezi na mhamasishaji wetu mkubwa Mw. Bakari Kombo Bakari.

Nne, kwa udhati wa moyo wangu napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpendwa Bw. Hemed Said Masoud, watoto wangu, Mariam, Hafidh na Salha Hemed Said Masoud. Nawashukuru wote Kwa kunipa msaada na kunitia moyo katika juhudi zangu za kimasomo pamoja na kunistahamilia pale nilipokuwa katika kipindi kigumu chote cha masomo yangu. Mungu awape kila lililo na kheri nao. AMIN.

Tano, napenda kutoa shukran zangu za dhati kwa uongozi wangu wa shule ya Sekondari ya Utaani. Namshukuru mwalimu mkuu Bi. Mwanakombo Nassor Amir kwa kunipa msaada mkubwa pale nilipokuwa nauhitaji. Vilevile sitakuwa mchache wa shukran kwa mwalimu mwenzangu, mwalimu Sharif Juma Fakih kwa kutumia muda wake mwingi kuniongoza na kujitolea kunisaidia katika kipindi chote cha masomo yangu. Nae, namuombea kwa Mungu ampe kile anachokihitaji chenye kheri nae, Amin.

Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wanachuo wenzangu wapenzi kwa kujenga mashirikiano, umoja, ushauri, nasaha na kunipa msaada mkubwa kila pale nilipokuwa nauhitajia kutoka kwao na kuwa pamoja katika juhudi zetu zote za masomo hadi kuikamilisha kazi hii. Miongoni mwa walionisaidi kwa ukaribu zaidi ni Maryam Said Masoud, Safia Said Msoud, Asha Khalfan. Nimewataja hao kwa niaba ya wengine ambao sikuwataja. Nawashukuru wote kwa nanma ya pekee kwa misaada yao ya namna moja au nyengine. Inshaallah Mungu awabariki. Amin.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu: Kuchunguza Fani na Dhamira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano Riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Utafiti ulikuwa na malengo mahsusi mawili, ambayo ni: Kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* na lengo la pili ni kuchambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Katika kutimiza malengo haya, mtafiti alikusanya data kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani na kufanya uchambuzi wa data kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Simiotiki na Sosholojia. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba, suala zima la malezi ya watoto ni changamoto kwa wazazi na jamii. Kwa lengo la kupatikana ufanisi wa malezi na maadili mema ni lazima pande mbili za familia zishirikiane kwa pamoja ili kujenga familia bora. Kwa ujumla ni matumaini ya mtafiti kufikisha vyema dhamira ya malezi na kuamsha ari kwa jamii na taifa kwa ujumla na kupelekea kushajihishika kuwalea watoto wetu katika maadili mema kwa faida ya familia, jamii na taifa kwa lengo la kuwa na taifa bora la baadae.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ ii

**HAKIMILIKI** ........ iii

**TAMKO** ........ iv

**TABARUKU** ........ v

**SHUKURANI** ........ vi

**IKISIRI** ........ viii

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ xiii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti ........ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 3

1.4.1 Lengo Kuu ........ 3

1.4.2 Lengo Mahsusi ........ 4

1.5 Maswali ya Utafiti ........ 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 4

1.7 Mawanda ya Utafiti ........ 5

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ........ 6

**SURA YA PILI** ........ 7

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ 7

2.1 Utangulizi ........ 7

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali ..... 7

2.2.1 Malezi ..... 7

2.2.2 Malezi ya Mtoto ..... 8

2.2.3 Mtoto ..... 8

2.2.4 Riwaya ..... 9

2.2.5 Fani ..... 10

2.2.6 Matumizi ya Lugha ..... 13

2.2.7 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Fani katika Riwaya ya Kiswahili ..... 14

2.2.8 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Dhamira ya Malezi katika Riwaya ya Kiswahili ..... 17

2.2.9 Mkabala wa Kinadharia ..... 21

2.3 Hitimisho ..... 28

**SURA YA TATU** ..... 29

**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ..... 29

3.1 Utangulizi ..... 29

3.2 Eneo la utafiti ..... 29

3.3 Usanifu wa Utafiti ..... 30

3.3.1 Sampuli ..... 30

3.3.2 Usampulishaji Lengwa ..... 31

3.4 Aina ya Data ..... 32

3.4.1 Data za Msingi / Awali ..... 32

3.4.2 Data za Upili ..... 33

3.5 Mbinu za Kukusanya Data ..... 33

3.5.1 Mbinu ya Usomaji Makini Kupitia Maktabani ..... 34

3.5.2 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka ........ 35
3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data ........ 35
3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 36
3.7 Usahihi wa Utafiti ........ 36
3.8 Maadili ya Utafiti ........ 37
3.9 Zana / Vifaa vya Utafiti ........ 38
3.9.1 Kalamu na Notibuku / Shajara ........ 38
3.9.2 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida ........ 38
3.9.3 Kompyuta na Wavuti / Tovuti ........ 38
3.10 Hitimisho ........ 39
**SURA YA NNE** ........ 40
**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI** ........ 40
4.1 Utangulizi ........ 40
4.2 Wasifu wa Mwandishi: Emmanuel Mbogo ........ 40
4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie ........ 42
4.4 Mbinu za Kisanaa katika Ujenzi wa Dhamira ya Malezi ya Watoto ........ 43
4.4.1 Mbinu ya Ujenzi Wa Mandhari ........ 43
4.4.2 Matumizi ya Mtindo ........ 50
4.4.3 Mbinu ya Ujenzi wa Wahusika ........ 60
4.4.4 Mbinu ya matumizi ya Lugha ........ 65
4.5 Dhamira ya Malezi Katika Riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie ........ 84
4.5.1 Malezi ya Watoto kwa Baba na Mama (Malezi ya Familia) ........ 85
4.6.1 Malezi ya Watoto kwa Majirani ........ 89
4.6.2 Malezi ya Watoto Shuleni ........ 95

4.6.3 Malezi ya Watoto kwa Vyombo vya Dola (Polisi) ........................................ 99

4.6.4 Malezi ya Watoto Mitaani ............................................................................ 101

4.7 Hitimisho ........................................................................................................ 105

**SURA YA TANO** ........................................................................................... 106

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............................ 106

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 106

5.2 Muhutasari ...................................................................................................... 106

5.2.1 Mbinu za kisanaa katika ujenzi wa Malezi ya Watoto ................................ 106

5.2.2 Dhamira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya Teule .................................. 107

5.3 Hitimisho ........................................................................................................ 107

5.4 Mapendekezo ................................................................................................... 108

**MAREJELEO** ................................................................................................ 109

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACRWC | African Charter on The Rights and Welfare of The Child |
| AMREF | African Medical and Research Foundation |
| FHI | Family Health International |
| LHRC | Legal Human Rights Center |
| MECPZ | Madrasa Early Childhood Program Zanzibar |
| N.K | Na kadhalika |
| PhD | Doctor of Philosophy |
| SW | Subhanahu Wataala |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UNCRC | The UN Convention on the Rights of the Child |
| UNICEF | United Nation International Children Education Fund |

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu wenye mada: Kuchunguza Fani na Dhamira ya Malezi ya watoto katika riwaya ya Kiswahili: Mfano riwaya ya *Watoto wa Mamantilie.* Katika sura hii, utafiti umejikita kufafanua vipengele vya msingi vifuatavyo: Usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti. Pia, mipaka ya utafiti, maadili ya utafiti na mpangilio wa tasnifu vimefafanuliwa vyema. Vipengele vyote hivyo ndivyo vinavyokamilisha utangulizi wa utafiti mzima. Ufafanuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

## 1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Utafiti huu umempa msukumo zaidi mtafiti kuhusiana na mada yake ya utafiti isemayo: Kuchunguza fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya Kiswahili: Mfano riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Dhana ya malezi bora hasa kwa watoto imemsaidia mtafiti kuweza kubaini matendo mbalimbali yakiwemo mema mfano, umuhimu wa matunzo, elimu na mapenzi kwa wazazi. Kwa upande wa matendo maovu yanayowakumba watoto katika maisha yao ni kama vile kukosa malezi hasa ya pande mbili, ambayo husababisha kubaguliwa, kutopatiwa haki ya elimu, kudhalilishwa, n.k.

Kupitia jarida la Kituo Cha Huduma za Sheria Zanzibar (2014), lenye mada isemayo: "Ufafanuzi wa Mikataba ya Haki za Watoto (UNCRC & ACRWC)" limeelezea

misingi ya mkataba wa kimataifa kuhusu watoto kuwa ni pamoja na: Mosi, Kutokuwepo ubaguzi: Watoto wote ni sawa na wanastahili kutendewa usawa. Pili, Watoto kwanza: Watoto ni rasilimali zinazolindwa na kuzalishwa kwa kuzingatia mahitaji ya watoto wa sasa na baadae. Tatu, Ushiriki: Ushiriki wao kulingana na uwezo wao kadiri wanavyokuwa.

Dhana hii, imelenga kutambua thamani ya mtoto na malezi anayotakiwa kupewa ili kumnusuru kujiingiza katika matendo maovu, na kumfanya ahukumiwe kwa taratibu au sheria stahiki. Jambo hili linaenda sambamba na mada ya mtafiti kwa kuzingatia umuhimu wa malezi bora kwa watoto na sio vyenginevyo ili kuwajenga kiimani kwa lengo la kupata familia na jamii iliyobora.

Suala la malezi ya watoto ni nyeti sana kwa kuzingatia umuhimu wao, hivyo mtafiti ameona kwa upande wa fasihi bado kuna haja ya kufanya utafiti kupitia malezi ya watoto, kwasababu tafiti nyingi zimegusia dhana ya malezi kwa ujumla mfano, Nafasi ya Mwanamke, malezi kwa vijana n.k, lakini utafiti unaohusiana na malezi ya watoto bado ipo haja ya kutafitiwa kwa kina zaidi. Watoto ndio kiini na muhimili katika maisha ya kila siku, ni kiumbe kinachokuwa, ni matarajio ya baadae katika kuuendesha ulimwengu na vilivyomo. Hivyo, mtafiti ameona kuwa ipo haja ya kufanya utafiti unaohusu fani na dhamira ya malezi ya watoto kwa lengo la kutambua uwepo wao, maendeleo na changamoto/vikwazo vinavyowakabili katika kuimarisha maendeleo yao na taifa kwa ujumla na kutoa mapendekezo ili kuondokana na vikwazo hivyo.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Mada kuhusu malezi ya watoto katika fasihi, imefanyiwa utafiti na baadhi ya wataalamu mbalimbali na kuibua mitazamo tofauti. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Kisanji (2013), Omar (2013), Msaki (2015), Ali (2015), Wanjala (2015), Fakih (2017) na wengineo. Kwa ujumla pamoja na kuwa watafiti hao wametafiti vipengele muhimu mbalimbali vikiwemo nafasi ya mwanamke na dhana nzima ya maadili, mada kuhusu malezi ya watoto bado haijatafitiwa kwa kina. Kwa mfano Omar (2013) kupitia tasnifu yake "Nafasi ya hadithi Simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari visiwani Zanzibar" Mtafiti amefafanua tabia mbalimbali wanazojifunza watoto kupata maadili mema, mfanon heshima kwa wazee, walimu na wengineo, kukuza vipaji vya akili, kusaidia kujua historia ya jamii inayofungamana na maadili mema katika utamaduni wao.

Kwa hivyo, mtafiti ameona iko haja kuchunguza nafasi ya malezi kwa watoto katika kutambua maendeleo na vikwazo na jinsi ya kuvikwamua vikwazo hivyo kwa kurejelea riwaya ya *Watoto wa Mama N'tiliye*. Mtafiti ameona kuna umuhimu wa kufanya utafiti huo kwa kuwa bado eneo hilo halijatafitiwa kulingana na mada ya mtafiti.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanywa sehemu mbili, Lengo kuu na malengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya Kiswahili: Mfano

riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.*

### 1.4.2 Lengo Mahsusi

i) Kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie.*

ii) Kuchambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie*?

**ii)** Ni dhamira zipi za malezi ya watoto zilizojitokeza katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Mtafiti anaamini kuwa utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika taaluma ya fasihi, kwa hiyo matokeo ya utafiti huu, yatachangia katika maarifa ya Kiswahili na fani nyenginezo kijamii, kitaaluma, kinadharia.

Kitaaluma, mtafiti anaamini kuwa utafiti huu utasaidia sana kuziba pengo la kiutafiti kuhusu malezi ya watoto ikizingatiwa ya kwamba watafiti wengi wametafiti kuhusu maadili kwa ujumla. Mada kuhusu malezi ya watoto bado inahitajika kutafitiwa. Hivyo utafiti huu utakuwa ni marejeleo muhimu kwa watafiti wengineo. Kinadharia, mtafiti anaamini kuwa ndani ya tasnifu hii itakuwa ni msaada mkubwa na adhimu

kupitia kipengele cha malighafi katika mada stahiki. Tasnifu hii itasaidia kuwa nyongeza katika nadharia mbalimbali zinazohusu nafasi ya malezi ya watoto ikiwemo matumizi sahihi ya nadharia ya Sosholojia.

Kijamii, Utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa kuongeza na kusisitiza thamani ya malezi ya watoto hususan kuwafunza maadili mema. Wazazi/walezi na taifa kwa ujumla, watanufaika vyema na utafiti huu, kwa kutambua juhudi za makusudi za kufanywa kwa lengo la kusimamia misingi madhubuti ya kuwalea watoto kuwa na maadili mema.Vilevile jamii ifahamu umuhimu na mchango wa malezi mema kwa watoto ili kujenga familia na taifa bora, lenye kufuata maadili na malezi yanayokubalika.

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti amejishughulisha na riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* ya mwandishi Emmanuel Mbogo. Utafiti huu umehusu fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule. Nadharia zilizotumika ni Simiotiki na Sosholojia. Nadharia ya Simiotiki, imetumika kwa lengo la kuchambua vipengele vya fani katika riwaya teule ambavyo ni: mandhari, mtindo, wahusika na lugha. Sosholojia imetumika kuchambua dhamira ya malezi ya watoto. Kwa ujumla mtafiti anaamini nadharia hizo zimeakisi vyema uchambuzi wa utafiti huu. Mtafiti anaamini kuwa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* imefaa sana kutimiza malengo na maswali ya utafiti kwa mujibu wa mada husika. Sambamba na hilo, mtafiti hatajishughulisha kuchambua vitabu vyengine vya mwandishi huyo, isipokuwa amevitumia pale ilipolazimu hususan katika mapitio ya kazi tangulizi na marejeleo mengine muhimu.

## 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ni Utangulizi wa jumla yenye vipengele: Usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili ni Mapitio ya kazi tangulizi na Mkabala wa kinadharia. Vipengele husika ni: Utangulizi, Ufafanuzi wa istilahi mbalimbali. Mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu ni Mbinu za utafiti. Vipengele vyake ni: Utangulizi, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo, usahihi wa utafiti, maadili ya utafiti, zana/vifaa vya utafiti. Sura ya nne ni: Uwasilishaji na Uchambuzi wa data. Vipengele vyake: Utangulizi, wasifu wa mwandishi Emmanuel Mbogo na muhtasari wa riwaya teule, uchambuzi wa mbinu za kifani. Uchambuzi wa dhamira ya malezi ya watoto na mwisho ni hitimisho. Sura ya tano ni: Hitimisho, Muhtasari na Mapendekezo.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imefafanua istiliahi muhimu na kurejelea kazi tangulizi mbalimbali kama tasnifu, machapisho, majarida, makala na vitabu vilivyohusiana na mada husika kwa minajili ya kupata maarifa, taarifa na data za ziada juu ya mada inayotafitiwa. Nadharia zilizotumika katika utafiti huu ni Simiotiki na Sosholojia. Kwa misingi hiyo sura hii imekuwa muhimu katika utafiti huu na ufafanuzi wa vipengele tajwa ni kama ifuatavyo:

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

Katika kipengele hiki istilahi kadhaa za kifasihi zinazohusiana na mada ya utafiti zimefafanuliwa, istilahi hizo ni Maana ya malezi na malezi ya mtoto, mtoto, riwaya, fani na vipengele vyake ambavyo ni: Mandhari, wahusika, mtindo, muundo na maana ya matumizi ya lugha.

### 2.2.1 Malezi

Neno malezi lina maana ya upekee katika jamii nyingi duniani, pia limeweza kutafsiriwa katika maana kadhaa. Jamal, (1980) anasema: Malezi ni amali aifanyayo mzazi kumlinda na kumuhifadhi mtoto kimaumbile kutokana na mazingira yaliyomzunguka. Pia anaendelea kusema kwamba; ni budi mzazi na jamii kuwa ni kigezo chema kwa watoto ili nao wapate kuiga mema kutoka kwao. (Tafsiri yangu).

Kwa ujumla, malezi ni taratibu zinazotumiwa na wazazi au walezi katika kusimamia misingi sahihi ya ukuaji wa mtoto. Lengo la malezi ni kumjenga mtoto katika tabia

njema zenye kukubalika na jamii husika zikiwa ni pamoja na elimu, maadili mema, mavazi, lishe na malazi bora.

### 2.2.2 Malezi ya Mtoto

Malezi ya mtoto ni mchakato wa maandalizi ya mtoto utakaomwezesha kupata maslahi bora. Malezi hayo humjenga mtoto kukua, kukubalika na kushiriki katika shughuli za kijamii na kiutamaduni kwa kumlinda, kumjamiisha na kumpatia huduma za msingi. Watoto wanatakiwa waonyeshwe malezi na njia nzuri wakiwa bado wabichi (wadogo), kwa kuanzia na upendo na kuthaminiwa kikamilifu kutoka kwa wazazi au walezi wao na jamii kwa ujumla.

Ingawa kuna changamoto kubwa katika malezi ya watoto na wakati mwengine husababishwa na wazazi/ walezi, hivyo basi wazazi/walezi bado wanajukumu kubwa la kuendelea kuwalea watoto katika maadili mema. Kwa upande wa fasihi nayo ina nafasi kubwa ya kuiongoza jamii wakiwemo watoto kuwa na maadili mema kama ilivyojitokeza katika riwaya teule ya *Watoto wa maman'tilie.*

### 2.2.3 Mtoto

Maana ya "Mtoto" imetolewa katika baadhi ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na sheria za nchi husika. Ibara ya 1 ya mkataba wa Umoja wa kimataifa wa Haki za Mtoto (UNCRC) wa mwaka (1989) na Ibara ya 2 ya mkataba wa watoto wa Afrika (ACWRC) uliotayarishwa mwaka (1990) imeeleza tafsiri ya mtoto kwamba ni binadamu yoyote aliye na umri chini ya miaka 18 isipokuwa kama sheria inayotumika inatambua umri wa utuuzima kabla ya hapo.

Maslahi bora ya mtoto ni mambo yote mema yenye kumuendeleza katika maisha yake. Hivyo msingi wa malezi ya mtoto unatakiwa kujengwa vyema tangu akiwa mdogo ili kuhakikisha kuwa, safari yake ya maisha inakwenda vyema.

### 2.2.4 Riwaya

Dhana kuhusu "riwaya" sio dhana ngeni katika ulingo wa Fasihi. Dhana hii imeelezwa na wataalamu mbalimbali kwa kina. Baadhi ya wataalamu hao ni kama hawa wafuatao:

Muhando na Balisidya (1976), wanaeleza kuwa riwaya ni kazi ya kubuni, ni hadithi ambayo hutungwa kufuatana na uwezo wa fanani kuibusha mambo kutokana na mazoea au mazingira yake. Waandishi hawa wanaendelea kusema kuwa riwaya yaweza kuanzia maneno 35000 hivi na kuendelea.

Ndungo na Mwai (1991), wanasema riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambavyo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kimaudhui na kifani. Mulokozi (1996) anaeleza riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.

Kwa ujumla riwaya ni moja kati ya utanzu wa fasihi andishi wenye masimulizi ya kubuni, lugha ya kinathari, mpangilio wa visa na matukio. Maneno katika riwaya yanaweza kuanzia 35,000, inayolenga jamii, na wakati husika, ikizingatia fani na maudhui iliyotimia.

### 2.2.5 Fani

Balisidya (1970) anasema, Fani ni kama kiumbiumbi cha nje cha fasihi na maudhui kama kiumbiumbi cha ndani. Msokile (1993) nae anaeleza, Fani ni umbo, ufundi au muundo wa kazi ya sanaa. Mambo kama lugha itumikayo, mtindo, muundo, mandhari nk. Fani pia ina maana ya tawi mfano, fani ya ushairi, hadithi fupi, tamthiliya na fani ya nyimbo.

Kwa kumalizia, Fani ni ufundi wa kazi ya kisanaa ambao msanii au mwandishi wa kazi ya fasihi huutumia katika kuipanga na kuipamba kazi ya fasihi. Fani ni msingi muhimu wa kuweza kufikia hatua ya kutambua Maudhui ya msanii. Fani hujengwa na vipengele vya msingi kama muundo, mtindo, mandhari, wahusika na matumizi ya lugha. Ufafanuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

#### 2.2.5.1 Mandhari

Cuddon (1979) anafafanua, mandhari ni mahali katika mazingira ya wakati fulani. Mahali na wakati husaidia kubainisha muktadha. Na muktadha husaidia kubainisha utamaduni wa jamii husika. Wamitila (2002) anaeleza, mandhari ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Madumulla (2009) anasema, mandhari katika kazi ya fasihi ni mahali ambapo tukio linatendeka.

Hivyo, mandhari ni jumla ya mahali, sehemu, kipindi, mazingira, au wakati ambapo matukio,/ visa, vituko na mikasa katika kazi ya msanii hufanyika. Mwandishi hukusudia kufikisha kwa jamii husika ili isawiri na uhalisia wa maisha ya jamii hiyo.

Mandhari katika kazi ya fasihi ni mahali ambapo tukio huandaliwa na mtunzi, mwandishi au msanii wa kazi ya fasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mandhari yanaweza kuwa halisi au ya kubuni (dhahania) katika kazi ya fasihi. Waandishi wengi hutumia mandhari halisi, inayoonekana na inayofikika na kuchanganya hapa na pale na ile ya kidhahania. Kwa mfano, mwandishi E. Mbogo katika riwaya yake ya *Watoto wa Mama N'tilie (2002)* ametumia mandhari ya halisi ya jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake.

**2.2.5.2 Wahusika**

Wahusika ni watu au hata viumbe vilivyochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria katika kazi yake (Ndungo na Mwai, 1991). Msokile (1993) anafasili, wahusika kuwa ni vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa; mfano katika kazi za fasihi kuna wahusika wanyama, watu, mimea n.k.

Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi, riwaya ikiwemo. Wahusika hawa wanaweza kuwa wanaadamu, wanyama, wadudu, madubwana, majini, mashetani, mawe na vitu vyengine visivyokuwa na uhai. Wamitila (2008) anafasili, mhusika kuwa ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanaadamu.

Kwa muhtasari, wahusika ni watu (binaadamu) au viumbe wengineo mfano wanyama, wadudu au vitu vyengine vinavyowakilisha matendo ya kibinaadamu.

Kwa ujumla mwandishi au msanii katika uga wa fasihi huwatumia kwa malengo ya kuibua dhamira na kufikisha ujumbe kwa jamii husika.

Aidha, wataalamu kadhaa wakiwemo Ndungo na Mwai, (1991), Msokile (1993) na Wamitila (2002) wameainisha aina mbalimbali za wahusika. Kwa ujumla mtafiti anaunga mkono aina kuu tatu za wahusika ambazo ni: Wahusika Wakuu, Wahusika Wadogo (Wasaidizi) na Wahusika Wajenzi. Mtafiti anaamini kuwa aina kuu hizi zimejitokeza katika kazi mbalimbali za fasihi ikiwemo riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Mtafiti kupitia aina hizo za wahusika amepata urahisi katika uchambuzi wake na kubaini matukio na dhamira zinazowasilishwa na mwandishi kupitia riwaya hiyo. Sambamba na hilo mtafiti anaamini wahusika ndio kisemeo au kipaza sauti cha mwandishi katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa.

### 2.2.5.3 Mtindo

Senkoro (1982) anasema, mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi, kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha nafasi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Vilevile anaeleza kuwa mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwengine asingeweza kuipa.  Hili linaweza kujitokeza hata kama jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lile lile moja.

Wamitlia (2003) anasema mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake, huelezea mwandishi anavyounda kazi yake. Dhana ya mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi

fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira, uakifishi wa sentensi, na kadhalika ndio yanayompambanua mwandishi huyu na mwenzake.

Kwa ujumla, mtindo hujikita na matumizi ya lugha, nafsi zilizotumiwa, matumizi ya monolojia / diolojia, igizo ndani ya igizo, taarifa za habari katika redio, maandishi katika mabango, kukopa msamiati kutoka lugha nyengine, picha na taswira, nyimbo, barua, hadithi ndani ya hadithi, n.k. Jambo la msingi katika mtindo ni lugha na ndiyo inayotofautisha fasihi na sanaa nyengine kama uchoraji, uchongaji, ufumaji, n.k. Msanii wa fasihi chombo chake ni lugha.

### 2.2.6 Matumizi ya Lugha

Msokile (1993) anaeleza kuwa, matumizi ya lugha ndiyo yanayofanya kazi fulani ionekane tofauti na nyengine au itofautishe kazi ya sanaa ya kifasihi na ile isiyo ya kifasihi. Lugha ndiyo mzizi wa kazi ya fasihi kwa kuwa fasihi ni kazi ya sanaa inayotoa maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno. Matumiziya lugha katika kazi ya fasihi yanajidhihirisha katika vipengele mbalimbali. Katika matumizi hayo kuna mambo kama tamathali za usemi, misemo, nahau, methali, lahaja, msamiati, miundo ya sentensi, uteuzi wa maneno, na kadhalika.

Jilala (2016) akimrejelea Senkoro (2011) anaeleza kuwa, lugha ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi kwa sababu ndio daraja linalounganisha hadhira na msanii katika mawasiliano. Katika kazi ya fasihi, lugha hubeba dhamira, migogoro na ujumbe mbalimbali alioukusudia mtunzi wa kazi hiyo ya fasihi. Ni kipengele

muhimu sana kwa sababu hutofautisha fasihi na sanaa nyengine kama vile uchoraji na uchongaji.

Kwa ujumla, lugha ndio roho ya kazi ya fasihi ambapo msanii au mwandishi huitumia kwa lengo la kufikisha maudhui yake kwa jamii husika kupitia utanzu teule. Kwa hakika, katika utafiti huu kipengele cha uchambuzi wa fani kina thamani kubwa kwa kuweza kufanikisha lengo mahsusi la kwanza linalokwenda sambamba na swali mahsusi la kwanza la utafiti huu. Uchambuzi wa vipengele hivyo umesaidia sana kudhihirisha uchambuzi unaofaa wa mbinu za kisanaa kwa kuzingatia mada ya utafiti huu. Mbinu hizo za kisanaa zimezingatiwa kwa mnasaba wa vipengele tajwa vya utafiti huu ambavyo ni Mandhari, mtindo, lugha na wahusika.

### 2.2.7 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Fani katika Riwaya ya Kiswahili

Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu fani yamesaidia sana kuimarisha utafiti huu. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa, Fani ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia mwandishi wa kazi ya fasihi katika kuisana kazi yake. Katika utafiti huu, mapitio ya kazi tangulizi kuhusu fani yametumika. Miongoni mwa hayo ni kama ifuatavyo:

Khatibu (1986) katika makala yake isemayo, Tamathali za usemi katika riwaya ya *Utengano* na *Nyota ya Rehema.* Pamoja na kujadili dhamira, utafiti huo umechambua kuwa watunzi wa riwaya hizo wametumia lugha ya kitamathali kama; tashhisi, ishara, mafumbo, taswira, tanakali sauti na tashibiha. Hivyo Khatibu (ameshatajwa) ameibua dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika utafiti wake ikiwemo nafasi ya mwanamke, umasikini na ndoa.

Makala ya Khatibu (ameshatajwa) imeusaidia sana utafiti huu, kwa kuwa dhana ya matumizi ya lugha ni kipengele muhimu katika fani. Matumizi hayo ya fani ndio msingi mmoja wapo wa utafiti huu.

Mulokozi (1990) kupitia makala yake isemayo: Utunzi wa Riwaya ya Kihistoria" Katika makala hiyo, ilieleza vipengele kadhaa vya Kifani na Kidhamira. Kwa upande wa fani makala hiyo ilichambua sifa za riwaya hasa za kihistoria,ambapo matokea katika mada hii, Mulokozi (ameshatajwa), katika mada yake amebaini vipengele vya fani kama Matumizi ya lugha, wahusika na mandhari.

Mchango wa makala ya Mulokozi (ameshatajwa), umekuwa na thamani katika utafiti huu kwa kuwa vipengele vya fani vilivyojadiliwa, ndio msingi muhimu katika kufanikisha mada ya utafiti huu kwa kurejelea riwaya ya *Watoto wa Mama N'tiliye*.

Mjema (1990) katika makala yake isemayo: Matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kusadikika".* Makala hiyo ilibaini kuwa mwandishi wa riwaya hiyo (Shaaban Robert) amezingatia matumizi ya lugha hasa kipengele cha tamathali za semi kuwa kimechangia sana katika kufanikisha dhamira ya riwaya hiyo. Miongoni mwa tamathali hizo ni tashibbiha, kejeli, taswira, tashihisi na sitiari.

Makala ya Mjema (ameshatajwa), imeendelea kuimarisha dhana ya matumizi ya lugha kama kipengele kimojawapo cha fani, kinachojadiliwa katika utafiti huu. Hivyo basi dhana inayojadiliwa ya fani imeendelea kuwa ni muhimu katika utafiti huu.

Kezilahabi, (1983) naye katika makala yake juu ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Makala hiyo, imebaini kwa kina juu ya umuhimu wa mtunzi katika ujenzi wa fani ili kufikisha maudhui yaliyokusudiwa. Miongoni mwa kipengele alichokisisitiza ni matumizi ya mandhari. Makala imesisitiza kuhusu mandhari halisia na isio halisia na matumizi yake.

Makala ya Kezilahabi (ameshatajwa) imeengeza uhai mkubwa wa utafiti huu, kwa kuwa dhana ya ujenzi mzuri wa fani, kikiwemo kipengele cha mandhari ndio msingi mmoja wapo maridhawa wa kazi ya fasihi.

Msacky (2015) katika tasnifu yake isemayo: Kuchunguza dhamira za kijamii na kisiasa katika riwaya ya *Siri za Maisha*. Katika tasnifu hiyo, imechambua dhamira mbalimbli kulingana na mada. Pamoja na mambo mengine, matokeo ya  utafiti huo ni kwamba, umebaini kwa kina mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumika ili kuibua dhamira. Mbinu hizo ni pamoja na, mbinu ya kishairi, sitiari, kidrama na misemo.

Kwa hakika utafiti wa Msacky (ameshatajwa) umeengeza ladha kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, mbinu za kisanaa zilizojadiliwa zimekuwa na tija kwa mnasaba wa  mada ya mtafiti. Kulingana na mada ya mtafiti, kipengele cha fani kimehusisha na matumizi ya mbinu za kisanaa, jambo ambalo limezingatiwa katika lengo la kwanza la utafiti huu.

Kimambo (2015) kupitia tasnifu yake isemayo; Kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za Kiswahili: Uchunguzi kifani wa riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

Utafiti huo ulichunguza na kuainisha matumizi ya tamathali za semi katika kipengele cha lugha. Utafiti wa Kimambo (ameshatajwa) uliendelea kubainisha matumizi ya lugha ya kitamthali za semi na isio ya kitamathali kupitia riwaya hizo teule.

Ni ukweli usiopingika, tasnifu ya Kimambo (ameshatajwa) imeengeza msaada mkubwa katika kufanikisha utafiti huu. Msaada huo umejitokeza kwa kuwa dhana ya matumizi ya lugha hasa ya kitamathali ni miongoni mwa vipengele muhimu katika matumizi ya lugha katika Fani. Kipengele cha Fani ni sehemu mojawapo ya lengo la kwanza la utafiti huu.

Kwa ujumla kazi tangulizi kuhusu fani, zimekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu kipengele cha fani ni nguzo muhimu ya uchambuzi wa lengo na swali la kwanza la mada ya utafiti huu isemayo: Kuchunguza fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya Kiswahili: Mfano riwaya ya *Watoto wa Mama N'tiliye.*

### 2.2.8 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Dhamira ya Malezi katika Riwaya ya Kiswahili

Katika utafiti huu, mtafiti amepitia kazi tangulizi mbalimbali kwa lengo la kutilia mkazo juu ya mada husika. Kazi tangulizi zilizorejelewa katika tasnifu hii ni pamoja na tasnifu, makala na majarida. Miongoni mwa kazi tangulizi hizo ni kama zifuatazo: Kezilahabi (1971), hakuwa nyuma katika kuandika dhamira ya malezi katika jamii ya Watanzania. Riwaya yake isemayo *Rosa Mistika*, ni riwaya iliyosheheni kwa kiwango kikubwa dhamira ya malezi kwa watoto ambapo suala la malezi

linalishughulisha sana taifa na dunia yake, kukabiliwa na vizingiti vingi kwa wazazi, jamii, taasisi za dini na elimu, masuala ya ulevi, umasikini, uvivu, mabadiliko ya wakati n.k, ni vikwazo kwa watoto katika malezi hasa katika nyakati za sasa.

Mtafiti, kwa kurejelea riwaya ya *Rosa Mistika* imekuwa na mchango mkubwa sana, kwa sababu imemsaidia mtafiti kupata data kuhusu malezi na athari ya kukosekana kwa malezi bora, kama madhara ya ulevi kwa wazazi, ikiwa ni miongoni mwa dhamira yake katika utafiti huu.

Wamitila (2008), ni miongoni mwa waandishi waliotafiti kuhusu riwaya Watoto wa maman'tilie. Mwandishi huyo ameeleza kuwa riwaya hiyo imesawiri uhalisia wa maisha ya wanawake hasa kupitia mhusika wake (Maman'tilie) ambae anafanya baishara ya kuuza genge la chakula huku akiandamwa na umasikini uliochangia kushindwa kuwapeleka watoto wake shule.

Mawazo haya yamekuwa msaada mkubwa kwa mtafiti, kwa sababu mada ya mtafiti inahusu fani na malezi ya watoto katika riwaya teule ya Watoto wa maman'tilie.Mtazamo wa Wamitila (ameshatajwa) umekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu, msingi wa mtazamo huo umemfanya mtafiti kuendelea kuchunguza kwa undani juhudi za wanawake hao katika harakati za malezi ili kujenga jamii iliyobora.

Omar (2013), kupitia tasnifu yake yenye mada: "Nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema katika skuli za upili visiwani Zanzibar". Mtafiti alichunguza

na kuainisha shida alizozipata mwanafunzi anaefundishwa maadili visiwani Zanzibar. Mtafiti aligundua mbinu mpya za kufundisha hadithi simulizi katika kufunza maadili visiwani. Hadithi ambazo zingewawezesha Wazanzibari wengi kujifunza hadithi simulizi kwa urahisi.

Tasnifu ya Omar (ameshatajwa) imekuwa msaada mkubwa kwa mtafiti, hususan katika kipengele cha malezi ikiwa maadili mema ni kiungo muhimu kwa mtoto katika kumkuza kimalezi. Dhana hiyo ya malezi ndio msingi muhimu katika utafiti huu.

Silau (2013), alitafiti kuhusu "Dhima ya nyimbo katika kukuza na kuimarisha malezi, akitoa mifano katika kabila la Wakaguru". Mtafiti aligundua dhima za nyimbo katika kabila hilo. Baadhi ya dhima alizozigundua ni: malezi mema, kujitambua na mmong'onyoko wa maadili.

Katika kuiangalia kazi ya Silau (ameshatajwa), mtafiti wa kazi hii amepata muongozo mzuri wa kazi yake, kwa sababu imemsaidia kuchambua dhamira ya malezi ya watoto kupitia riwaya teule, ili kuweza kubaini usadifu wa malezi hayo ulivyojitokeza katika riwaya hiyo kwa ukamilifu wake. Na kuzingatia kuwa suala la malezi ni jukumu nyeti katika jamii ya watanzania na dunia kwa ujumla.

Mzee (2015) alitafiti kuhusu "Kuchambua maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya wapemba". Mtafiti alibaini dhamira mbalimbali kama, ugumu wa upatikanaji wa elimu, umoja na mshikamano miongoani mwa wanajamii,

mapenzi na ndoa, kuonya, ukarimu, uzembe na uvunjaji wa kanuni , nafasi ya mwanamke pamoja na utawala bora

Kazi ya Mzee (ameshatajwa), imempa fursa mtafiti ya kumuongoza na kuendelea kutafiti dhamira ya malezi ya watoto, kupitia riwaya teule. Sambamba na hilo, tasnifu hiyo imekuwa na msaada mkubwa kwa mtafiti, ikizingatiwa mada kuhusu malezi ya watoto bado inahitajika kutafitiwa ili iendelee kuwa muongozo mwema wa kujenga jamii iliyo bora kama ambavyo mtafiti alivyojikita katika malengo na maswali ya utafiti huu.

Wanjala (2015) alitafiti "Usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili". Mtafiti aligundua na kuziainisha changamoto kadhaa kama vile; dhulma na unyanyaswaji wa vijana, madhara ya ulevi, ujasiri kama wasifu wa vijana na elimu. Mtafiti pia, amebainisha wahusika vijana wa jinsia zote walivyotelekezwa katika jamii.

Changamoto hizo, zilizojitokeza ndani ya utafiti wake zimekuwa na msaada mkubwa katika utafiti huu na zimesaidia sana kubaini changamoto kama hizo kwa malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Hivyo basi, utafiti huu ni kigezo muhimu na chenye thamani kubwa.kwa mtafiti ili kuweza kutambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule.

Msacky (2015) alitafiti kuhusu, dhamira za kijamii na kisiasa katika riwaya ya *Siri za Maisha*. Mtafiti huyu amezungumzia dhamira mbalimbali zikiwemo, umasikini, ulevi, uvivu, uzembe na nafasi ya mwanamke katika jamii.

Kazi hii imempa mwanga mtafiti katika kutimiza malengo na maswali yake ya utafiti. Pia, kazi hiyo imekuwa msaada mkubwa, kwa sababu imezungumzia malezi kwa ujumla wake kupitia vipengele hivyo. Utafiti wa Msacky (ameshatajwa), umekuwa ni muhimu na kufaa sana kwa mujibu wa mada ya mtafiti ambayo imelenga kuchambua mada ya malezi ya watoto.

Kimambo (2015) katika mada yake "Kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za Kiswahili: Uchunguzi kifani wa riwaya za Vipuli vya Figo na Siri za Maisha" Mtafiti huyo amejadili kwa kina dhamira kama biashara haramu, umuhimu wa elimu, malezi katika jamii, nafasi ya mwanamke na hali ngumu ya maisha.

Hivyo nafasi ya malezi imejitokeza kwa namna nyengine kupitia dhamira alizozichambua mtafiti, kama alivyobaini suala la matumizi ya dawa za kulevya na umasikini kuwa ni miongoni mwa vikwazo katika jamii. Maelezo hayo yamemsaidia sana mtafiti kuelewa changamoto za malezi. Hii ni kutokana na kwamba katika riwaya ya *Watoto wa MamaN'tilie* suala la malezi limesawiriwa na lina umuhimu mkubwa kwa jamii. Kwa ujumla mtafiti amesoma vitabu, tasnifu, majarida na mitandao mbalimbali na ameona kuwa ipo nafasi ya kufanya utafiti kuhusu malezi ya watoto katika riwaya ya Kiswahili, mfano riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tile.* Kazi tangulizi hizi zimemsaidia sana mtafiti kumuelekeza na kumuimarisha katika utafiti huu.

### 2.2.9 Mkabala wa Kinadharia

Neno "Nadharia" ni dhana yenye uwanja mpana. Wataalamu wengi wamejadili

dhana hii kwa mapana na marefu kwa mujibu wa mitazamo yao. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

Msokile (1993) anaeleza, Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Wamitila (2002), Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia. Wafula na Njogu (2007), Nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

Kwa ujumla, Nadharia ni jumla ya njia, maelekezo, mpango, muongozo unaomsaidia mtafiti au mhakiki na msomaji kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum. Katika utafiti huu, mtafiti amezingatia ufafanuzi na uchambuzi wa data za utafiti akihusisha na Nadharia ya Simiotiki na Sosholojia. Mtafiti anaamini kuwa nadharia ya Simiotiki ni muwafaka kwa kufanikisha lengo na swali la kwanza la utafiti huu, kwa sababu mtafiti ameona kwamba nadharia ya Simiotiki imejikita katika matumizi ya ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi, ambapo kipengele cha ishara kinahusiana na matumizi ya fani katika fasihi. Vilevile nadharia ya Sosholojia imefanikisha lengo na swali la pili la utafiti huu ipasavyo kulingana na mada ya utafiti. Hivyo mtafiti ameona iko haja ya kutumia nadharia zote mbili ili kukidhi lengo la utafiti wake.

#### 2.2.9.1 Nadharia ya Simiotiki

Wamitila (2002) anafafanua kuwa, simiotiki ni neno la kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki.

Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishuhulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi. Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii kiuchumi , kisisasa, na kiutamaduni.

Brown (1995) anasema kuwa, ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Ili watu waelewe kinachowasilishwa na ishara fulani, lazima watu hawa wawe na makubaliano fulani ambayo hutokana na kushiriki elimu, utamaduni, dini na mandhari sawa. Ishara hizi hujumuisha picha, rangi, maumbo mbalimbali na hata herufi zinazounda maneno. Watu wa asili tofauti huweza kuelewa ishara sawa kwa njia tofauti kutegemea tajriba zao ilhali watu kutoka jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni sawa huwa na ukubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake.

Miongoni mwa waasisi wa nadharia ya simiotiki ni Ferdinand de Saussure (1857 - 1913), Charles Peirce (1839-1914) na Rolland Barthes (1915-1980). Pierce (1958) wanaeleza: Simiotiki kama kanuni za ishara zinazowakilisha mtu au kitu katika hali fulani.

Nadharia hii ina misingi yake katika imani kuwa watu katika jamii moja wanaozungumza lugha moja na kuwa na utamaduni sawa huweza kuwasiliana kwa njia fiche. Katika kuchunguza athari za nadharia ya Simiotiki kwa jamii, Krawsczyn (2006) anadai kuwa nadharia ya Simiotiki inaweza kuleta mabadiliko katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii kwa kuwa itawatia motisha wanajamii

kuchunguza mazingira yao kwa jicho pekuzi huku wakizingatia kuwa kila ishara haikosi maana. Isitoshe, Simiotiki itawafanya wanajamii kuwa makini zaidi wanapoelewa kuwa ishara ndogo au sahili ina uwezo wa kubeba ujumbe muhimu. Kama mawasiliano ni mchakato wa kueneza habari kutoka chanzo chake hadi kwa anayeipokea, basi nadharia hii ya Simiotiki inahusu kueneza ujumbe uliosimbwa kwa kutumia ishara.

Nadharia ya Simiotiki haiwezi kukamilika bila kurejelea mawazo ya Barthes (1968) kuhusu misimbo mitano ya usomaji, ambayo imeacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uwashiriaji katika kazi za kifasihi. Misimbo hii ni miongoni mwa nguzo kuu za nadharia ya Simiotiki. Barthes (ameshatajwa) alidhamiria kugawanya kazi ya kifasihi katika vitengo vidogovidogo vyenye urefu sawa alivyoviita leksia na kwamba kila leksia ilidhihirisha faida yake muhimu katika kuifasiri. Barthes alifafanua misimbo ifuatayo:

**Msimbo wa matukio:** Msimbo huu unahusu namna matukio yanavyopatikana katika hadithi yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi.

**Msimbo wa kihemenetiki:** Msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi. Kwa hivyo huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi.

**Msimbo wa ki-seme:** Msimbo huu hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

**Msimbo wa kiishara:** Msimbo huu unahusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihii.

**Msimbo wa kiurejelezi:** Msimbo huu hujegwa kutokana na viashiria vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi ya fasihi. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo za kuitamaduni. Msemaji akisema kuwa anakielewa kitu anachokimaanisha msanii husema hivyo katika msingi wa kiurejelezi au kiutamaduni.

Tunaposoma kazi za fasihi tunakutana na matumizi ya lugha ambayo yanajenga misimbo ya aina hizo tano. Kwa mfano, msimbo wa kimatukio hujitokeza, kwa mtunzi wa kazi ya fasihi kujenga tukio linalofanywa na wanyama kama vile, mbwa, fisi, paka na ng'ombe ambapo kwa msomaji huweza kujenga taswira, ishara na picha ambazo zitampatia dhamira stahiki, Cobley (2001). Hivyo, tunakubaliana na maelezo kuwa, Simiotiki ni taaluma ya mfumo wa matumizi ya alama au ishara kwa nia ya kuwasiliana kati ya wanajamii na kuelewana baina yao.

Mtafiti ameamua kuchagua nadharia ya Simiotiki akiamini kuwa imekuwa ni nadharia muwafaka katika kutimiza shauku na kiu ya utafiti huu na kufanikisha lengo na kujibu swali la msingi la kwanza la utafiti huu ambalo limelenga katika mbinu za kisanaa. Nadharia ya Sosholojia ni nadharia ya pili adhimu itakayotumika ili kuweza kufanikisha lengo na kujibu swali la pili la utafiti huu ambalo linahusu dhamira ya malezi ya watoto. Maelezo ya nadharia hiyo ni kama ifuatavyo:

#### 2.2.9.2 Nadharia ya Sosholojia

Nadharia ya Sosholojia ni nadharia inayohusishwa na mwanasholojia Adam Smith (1970), kama ni muasisi wa nadharia hii huko Marekani. Nadharia hii imejikita zaidi na uhusiano wa mwanadamu na jamii yake, kwani nadharia hii inaonyesha jinsi wasomi wanavyoipokea, kuitathimini, na kuihukumu kazi fulani ya kifasihi huathiriwa pia na mazingira ya wasomaji hao. Mfano Msokile (1992) anaeleza kuwa nadharia ya Sosholojia huikabili kazi ya kifasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii. Nadharia hii inaamini kuwa uhusiano wa kazi ya kifasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Anazidi kufafanua kwamba kazi ya sanaa, haijengwi katika Ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira maalum akiwajibika kwa jamii inayomhusu ambayo ni sehemu yake muhimu. Mkabala huu kimsingi hutawaliwa na imani kuwa uhusiano katika kazi ya kifasihi na jamii ambayo kwa kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Mazingira ya jamii ndiyo yanayoweza kubadili maudhui ya kazi ya fasihi.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa nadharia ya Sosholojia inafungamanisha fasihi na jamii. Hii inaonyesha kuwa Sosholojia ni kielelezo cha hali halisi ya jamii na inachukuliwa kama zana mojawapo ya kijamii katika mazingira yake yaliyomzunguka. Nadharia hii inasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii. Msanii anachukuliwa kama mmoja katika jamii na mwenye nafasi yake katika jamii hiyo.

Naye Ntarangwi (2004) anasema kwamba, mtunzi mwenyewe ni mwanajamii kwa maana kwamba ana nafasi na tabaka fulani katika jamii yake; yeye hutambuliwa na

jamii kama mmoja wao. Hawezi kuepuka nafasi yake katika jamii wala hawezi kukwepa athari ya jumuiya katika utunzi wake kwani kama mtoto mchanga yeye hufundishwa maadili na itikadi za jamii yake ili kuweza kuzieneza katika jamii hiyo. Na kama ambavyo tumetaja tayari, mtunzi hulenga hadhira fulani hata iwe ndogo vipi.

#### 2.2.9.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Sosholojia

i) Umahsusi na sio Umajumui Ilikuwa mahususi zaidi kuliko nadharia zilizotangulia: badala ya kujikita katika taaluma ya sanaa jadi kwa ujumla (maumbile ya mwanadamu na utamaduni wa mwanadamu) kama walivyofanya wanadharia wa zamani, nadharia ya usosholojia ilijikita katika jamii peke yake. ·

ii) Muhimili unaokuza mahusiano/mashirikiano mema baina mtu, watu, jamii na taifa kwa ujumla

iii) Muhimili unaohusu umuhimu wa elimu na maendeleo kwa jamii

iv) Muhimili unaomuhusisha mzazi kuwa ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora,(uhusiano wa mzazi na mtoto)

v) Muhimili unaokuza mahusiano ya serikali, vyombo vya dola na jamii.

Nadharia hii imetumika katika utafiti huu kwa sababu, mada ya fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* imesaidia sana, hasa ukizingatia kwamba, masuala ambayo mwandishi E. Mbogo ameyaeleza ndani ya riwaya yake hii yamejikita zaidi katika masuala ya kijamii na kiuchumi pamoja na maendeleo ya watu ikiwa ni pamoja na malezi ya watoto.

Kwa mfano mwandishi amemchora Maman'tilie kama mama kiongozi ambae alijitahidi sana kutatua migogoro iliyojitokeza katika familia yake, mfano kati yake na mumewe, kuwahudumia watoto wake kupata elimu. Pia mwandishi katuonyesha jinsi Maman'tilie alivyofanya kazi kubwa sana ya kuuza chakula gengeni kwa maslahi ya familia yake. Nadharia hii imemsaidia mtafiti sana katika kuchunguza dhamira ya malezi ya watoto, hasa kwa kuwa riwaya nzima inahusu matatizo ya watoto katika maisha yao ya kila siku, athari walizozipata watoto hao katika mambo mbalimbali yaliyoizunguka jamii hiyo yakiwemo kukosa elimu, wizi, ulevi, madawa ya kulevya na ajira za utotoni.

## 2.3 Hitimisho

Kwa kuhitimishia, sura hii imekuwa na thamani kubwa katika kazi hii kwa sababu imeendelea kuipa uhai zaidi kwa kuelezea mambo ya msingi yanayohitajika katika utafiti huu. Mambo ya msingi yaliyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mwisho mkabala wa kinadharia. Huu ni mwendelezo mzuri wa kufikia hatua ya kufanikisha malengo na maswali ya utafiti ambapo ndio roho ya mada husika. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii mtafiti amekusudia kufafanua mambo ya msingi ambayo anaamini yamechangia vyema katika kufikia hatua nzuri ya uchambuzi wa kazi hii husika. Vipengele ambavyo vimejadiliwa ni: eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, usahihi wa utafiti, maadili ya utafiti na hitimisho. Kwa ujumla vipengele vyote ni muhimu na uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:

## 3.2 Eneo la utafiti

Utafiti huu umefanywa maktabani. Utafiti umelenga kukusanya data kutoka matini kadhaa zenye manufaa, kwani mtafiti ameweza kusoma vitabu, majarida, vitini, tasnifu mbalimbali kuhusiana na mada husika, jambo ambalo limemuwezesha mtafiti kukusanya data zake vizuri. Utafiti umekusanya data kutoka katika maeneo kadhaa kama: Pemba, mfano, Maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania – tawi la Pemba, Maktaba kuu Zanzibar - tawi la Pemba iliyopo wilaya ya Chakechake, maktaba ya wilaya ya Wete, Maktaba ya shule ya sekondari Utaani. Maeneo haya yamekuwa karibu na mtafiti na kumuwezesha kukusanya data kwa urahisi. Pia mtafiti amekusanya data kupitia wavupepe / tovuti, magazeti, redio, ripoti za tafiti zilizokusanywa ambapo taarifa hizo zimefanana na mada iliyofafanuliwa na kupata taarifa ambazo zimemsaidia mtafiti kufikia malengo na maswali ya utafiti wake vizuri na kwa usahihi.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu umetumia mkabala wa kimaelezo. Mtafiti amekusanya data na kuzichambua kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mbinu ya tarakimu huwa haitumiki. Hivyo data katika utafiti huu zimekusanywa na kuchambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo. Sambamba na hilo, mbinu zilizotumika kukusanya data ni usomaji makini kwa data za awali. Data hizo zimekusanywa kupitia riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Kwa upande wa data za upili zimekusanywa kwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka mbalimbali zikiwemo, tasnifu, makala, vitabu, tovuti zenye uhusiano na mada ya utafiti.

Mtafiti ameteua riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* akiamini inafaa na inatosha kufanikisha vyema malengo na masuali ya utafiti. Mbinu alizozitumia mtafiti zimemrahisishia sana mtafiti kupata data anazozihitaji hii ni kwa sababu mbinu hizo hazimfanyi mtafiti kutumia muda mwingi katika utafutaji wa data. Vilevile matumizi mazuri ya muda yamemsaidia sana mtafiti kumaliza tasnifu hii katika muda muafaka pasi na kuchoshwa. Bila shaka mbinu hizo ni bora katika utafiti huu.

### 3.3.1 Sampuli

Katika utafiti dhana ya sampuli na usampulishaji ni dhana pana na muhimu ambapo watafiti mbalimbali wamefafanua kulingana na mitazamo yao. Miongoni mwa fasili hizo ni kama ifuatavyo:

Kothari (1990, 2004) anaeleza, Sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake.

Bryman (2004) anafafanua, Uteuzi wa Sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima.

Kwa ujumla sampuli ni kundi dogo la watu au vitu linaloteuliwa kutoka kundi kubwa la watafitiwa kuwakilisha sifa, tabia za kundi zima kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Hivyo ni kusema kwamba, sampuli ni sehemu ndogo ya watafitiwa inayoteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuwa kiwakilishi cha hilo lote. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia sampuli lengwa katika ukusanyaji wa data kulingana na mada.

### 3.3.2 Usampulishaji Lengwa

Usampulishaji lengwa ni miongoni mwa mbinu adhimu katika ukusanyaji wa data za utafiti kulingana na mada husika.

Yin (1994) anafafanua kuwa, usampulishaji lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti anateua watafitiwa ama vitafutiwa akiwa amejiridhisha kwamba watafitiwa hao watampatia data itakayoweza kutimiza malengo ya utafiti wake. Babbie (1999) anaeleza, Usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti kwa wepesi na haraka.

Mbinu ya usampulishaji lengwa imetumika katika utafiti huu kwa kuteua riwaya ya *Watoto wa MamaN'tilie* ya mwandishi Emmanuel Mbogo. Mtafiti amejiridhisha na

kuamua kutumia mbinu hiyo akiwa na imani kubwa ya kwamba inafaa na inatosha katika ukusanyaji wa data anazozihitaji kulingana na mada. Marejeleo mengine yametumika kwa lengo la kutilia mkazo na kujenga ufanisi katika utafiti huu.

### 3.4 Aina ya Data

Utafiti huu umelenga kukusanya data za msingi na data za upili. Data za msingi ni kutoka katika riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie* (2002). Kwa upande wa data za upili, mtafiti amedurusu matini mbalimbali zinazohusiana na mada yake, mfano, kusoma kwenye mitandao kazi zinazo husiana na mada, kupitia tasnifu mbalimbali zilizojadili suala la malezi na vipengele vya fani, vitabu, majarida na makala kadhaa zinazohusiana na mada teule, ambapo data zote hizo zimemsaidia mtafiti.

#### 3.4.1 Data za Msingi / Awali

Wataalamu mbalimbali wameeleza fasili ya data za awali/msingi. Miongoni mwao ni: Kothari (2004) anaeleza kuwa, Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi. Adam na Kamuzora (2008) wanabainisha, Data za awali ni aina ya data zilizokusanywa na mtafiti mwenyewe au msaidizi wa mtafiti kutoka katika eneo halisi kwa lengo la kujibu maswali au mada ya utafiti.

Kwa muhtasari, Data hizi za msingi hazijapata kukusanywa na mtafiti mwengine yeyote kwa dhamira ya utafiti kama huu ambao umekusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza. Katika ukusanyaji wa data za msingi, mtafiti amesoma na kuchanganua riwaya teule, ili kupata maelezo kuhusu fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* (2002). Uchunguzi wa kina mtafiti ameufanya

akihusisha na nadharia ya Simiotiki na Sosholojia ambazo anaamini zimemwongoza vyema katika utafiti wake.

### 3.4.2 Data za Upili

Kwa upande wa data za upili, wataalamu wamefafanua kama ifuatavyo: Kothari (2004) anasema, Data za Upili ni data zote ambazo tayari zimekwisha kusanywa na mwingine na ambazo zimepatikana katika hatua zote stahiki za ukusanyaji wa data. Kamuzora na Adam (2008) wanaeleza, data za upili ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengineo kwa lengo maalum.

Kwa ujumla, Data za upili ni aina ya data katika utafiti ambapo mtafiti huzikusanya kutoka vyanzo mbalimbali zikiwa tayari zimeshakusanywa na mtafiti mwengine. Mtafiti ametumia data za upili kupitia maeneo mbalimbali. Mtafiti amekusanya data hizo katika : Maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT), Maktaba ya chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Maktaba ya chuo kikuu cha Zanzibar (ZU) na Maktaba kuu ya Zanzibar. Maktaba zote hizo zinapatikana visiwani Pemba ikiwa ni matawi. Pia mtafiti amekusanya data kupitia tasnifu, wavupepe / tovuti, magazeti, majarida , ripoti na makala mbalimbali zenye uhusiano na mada teule.

## 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (1990) anasema, Mbinu za ukusanyaji data ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanyia data kwa ajili ya utafiti wake. Bailey (1994) anabainisha, Mbinu za kukusanyia data ni mbinu za kifalsafa za mtafiti ambazo zinakuwa na

mabunio kulingana na kazi yake mtafiti, na jinsi atakavyoweza kukusanya data hizo, kuzichambua na kuandika taarifa ya matokeo ya utafiti.

Hivyo basi kwa ujumla, mbinu za kukusanyia data ni ujuzi na ufundi autumiao mtafiti na kumsaidia kukusanya data anazozihitaji. Katika utafiti huu mbinu ya usomaji makini kupitia maktabani na mbinu ya upitiaji wa nyaraka zimetumika kwa yakini ili kumuwezesha mtafiti kwa kiasi kikubwa kukusanya data zake

### 3.5.1 Mbinu ya Usomaji Makini Kupitia Maktabani

Enon (1998) anaeleza, Mbinu ya usomaji makini ni mbinu inayomtaka mtafiti kukusanya taarifa kwa umakini baada ya kusoma kwa kina kazi husika kunzia mwanzo hadi mwisho. Kothari (2004) anasema, Usomaji makini ni mbinu inayolenga kusoma na kuchambua kwa undani (kwa kina) maudhui yanayojitokeza katika kazi husika kama vitabu, majarida, magazeti yanayoendana na mada husika.

Mbinu hii ya usomaji makini kupitia maktabani, mtafiti amesoma kwa makini na kwa udadisi mkuu kazi mbalimbali katika maktaba ambazo zinahusu mada yake. Katika mbinu hii mtafiti ametumia mbinu ya usomaji makini, kupitia kitabu husika ambacho ni *Watoto wa Mama N'tiliye,* huku akiwa na matarajio makubwa ya kupata taarifa za uhakika katika utafiti huo.

Kwa kupitia njia ya maktabani, mtafiti ametumia mbinu hii ya usomaji makini ili kujiridhisha hatua baada ya hatua mpaka mwisho wa riwaya yake teule ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Mtafiti amevipitia kwa undani vipengele vya fani kama: muundo,

mtindo, mandhari na lugha na kunukuu aya kadhaa zitakazohusiana na dhamira ya malezi na mbinu za kifani katika riwaya teule kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti.

### 3.5.2 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kutoka katika machapisho mbalimbali yanayopatikana maktabani (Young, 1984). Maktaba ni chanzo sahihi na muhimu ambapo hupatikana na machapisho ya aina mbalimbali. Mtafiti amefanya upitiaji wa nyaraka katika maeneo kadhaa mfano, Maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT), Maktaba ya chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Maktaba ya chuo kikuu cha Zanzibar (ZU). Maktaba zote hizo zinapatikana visiwani Pemba ikiwa ni matawi. Pia mtafiti amekusanya data kupitia tasnifu, wavu pepe/ tovuti, magazeti, majarida, ripoti na makala mbalimbali zenye uhusiano na mada ya mtafiti.

## 3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Babbie (1999) anasema kuwa, Data zinazokusanywa wakati wa utafiti hazina budi kufanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti na malengo ya utafiti yaliyokusudiwa.

Hivyo ni kusema kuwa, mtafiti katika uchambuzi wa data, ambao umemuwezesha kukusanya data zilizohalali na kuzichambua. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo. Mkabala huo umemuwezesha mtafiti kuchambua data kwa minajili ya kufanikisha malengo na masuali yake ya utafiti na kupata

matokeo sahihi. Baada ya kupitia matini teule na kuangazia mbinu za kisanaa na dhamira ya malezi ya watoto, mtafiti amechanganua kwa kina masuala na malengo ya utafiti kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

### 3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo

Kothari (1990) anaeleza kuwa, Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mbinu hii imemuwezesha mtafiti kwa umakini kukusanya data kwa kutumia madondoo, kufafanua na kutolea maelezo. Mbinu hii imekuwa bora na imemuwezesha mtafiti kuwa na umakini wa kukusanya data, kwa kutumia madondoo, kufafanua na kutolea maelezo. Sambamba na hilo, mtafiti amezingatia uteuzi wa matumizi ya nadharia sahihi ya Simiotiki na Sosholojia. Mtafiti ameonelea uhusishaji wa nadharia hizo zimemsaidia kufanikisha vyema malengo na kujibu maswali yake ya utafiti. Kwa ujumla uchambuzi wote wa data umeenda sambamba na mada ya utafiti isemayo: Kuchunguza fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*.

## 3.7 Usahihi wa Utafiti

Kwa nia safi, heshima, na taadhima kubwa, mtafiti anaamini kwamba data zote zilizokusanywa zimekuwa sahihi na za uhakika kabisa, hii ni kwa sababu zifuatazo:

Mosi, mtafiti alipitia na kusoma kwa usomaji makini riwaya teule, majarida, makala mbalimbali, pamoja na kukusanya data za ukweli kwa kuzifanyia uchambuzi yakinifu na uhakika huku akiamini kwamba data hizo zimemsaidia vya kutosha katika kutoa majibu sahihi ya maswali yake ya utafiti. Pili, mtafiti amepitia mitandao

mbalimbali kama, wavupepe, na kusikiliza vyombo vya habari kama redio kupata data kwa mujibu wa mada yake inayohusiana na malezi ya watoto, ambapo amefaidika kupata na kukusanya maarifa na data zinazohusiana na mada yake na kuweza kumsaidia vya kutosha katika utafiti wake.

Mwisho, mtafiti ana imani kupatiwa fursa muhimu na adhimu ya kupitiwa na kusomwa kwa utafiti huu na msimamizi wake, kumempa fursa na uweledi mkubwa na kumpanulia mawazo kitaaluma kwa kuweza kufanikisha utafiti wake kwa kufuta maelekezo aliyopewa na kurekebishiwa kasoro zilizojitokeza ndani ya utafiti huu.

## 3.8 Maadili ya Utafiti

Tamko la Nurenberg (1974) linasema, Maadili ya utafiti yanahusu matumizi mazuri, kanuni bora, uadilifu kwa mtafiti na watafitiwa na katika mada yenyewe. Kuna masuala mengi ya kimaadili ambayo yanahitaji kutiliwa maanani kwa utafiti, moja ni kulinda usalama, uaminifu, kufahamu majukumu ya watafitiwa, na nidhamu bora ya kazi.

Seture (2010) anaeleza mkabala wa maadili ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti alipaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Mtafiti amezitambua haki zote nakuzifanyia kazi, ambapo palipotokea tatizo mtafiti amechukua dhamana itakayostahiki.

Mtafiti ametumia eneo la maktabani, na katika maeneo mengine kama vile shuleni, nyumbani na chuoni. Katika sehemu zote hizo sheria na kanuni, maadili,

silka zimezingatiwa. Katika utafiti huu mtafiti amejitahidi kutekeleza maadili, kanuni na taratibu stahiki za kiutafiti ili kuhakikisha ukusanyaji wake wa data umekuwa sahihi na uhakika ili kumuwezesha kujibu maswali yake ya utafiti vyema na inavyostahiki.

## 3.9 Zana / Vifaa vya Utafiti

Mulokozi (1983) anaeleza: Vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivyo huwa ni pamoja na: Kalamu na Karatasi, Shajara, Tepu rekoda (kirimbo) na vifaa vyake, Video (pataninga); na vifaa vyake, Kamera na vifaa vyake, Ngamizi na vikorokoro vyake. Vifaa vya kupimia na kuhesabia. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia vifaa vifuatavyo:

### 3.9.1 Kalamu na Notibuku / Shajara

Vifaa hivi vimetumika kwa ajili ya kuandikia taarifa mbalimbali kwa lengo la kuweka kumbukumbu za taarifa ambazo zimekusanywa katika mfumo wa maandishi zinazohusiana na mada, malengo na maswali ya utafiti.

### 3.9.2 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida

Vifaa vyote hivi vina umuhimu mkubwa katika utafiti huu.Vifaa hivi vimetumika kama ni sehemu muhimu ya kurejelea wakati mapitio ya kazi tangulizi pamoja na ufafanuzi wa mambo muhimu katika uchambuzi wa data za utafiti ili kuufanya utafiti huu utosheleze mahitajio ya malengo na maswali ya utafiti.

### 3.9.3 Kompyuta na Wavuti / Tovuti

Kompyuta imetumika kwa kiwango kikubwa kuchapa kazi hii ya utafiti kuanzia

mwanzo hadi mwisho. Wavuti / Tovuti zimetumika kwa lengo la kutafutia machapisho, maarifa, tasnifu na taarifa nyenginezo muhimu zenye kuhusiana na mada ya utafiti.

### 3.10 Hitimisho

Kwa ujumla mtafiti ameelezea na kuchambua vipengele vya msingi vilivyomsaidia katika kufikia hatua nzuri ya utafiti wake. Vipengele vilivyochambuliwa ni pamoja na hivi vifuatavyo: Maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data zitakazokusanywa, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, usahihi wa utafiti pia na maadili ya utafiti yalielezwa kitu ambacho kimemsaidia katika kuweka bayana uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura inayofuata imehusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imebeba vipengele vya msingi vifuatavyo: utangulizi, wasifu wa mwandishi E. Mbogo, historia ya riwaya teule, uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Data za utafiti zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa kuzingatia malengo mahsusi na maswali ya utafiti. Katika lengo mahususi la kwanza linalokwenda sambamba na swali la kwanza na nadharia ya Simiotiki imetumika. Nadharia ya Sosholojia imetumiwa kwa lengo mahsusi la pili linalowiana na swali la pili.

## 4.2 Wasifu wa Mwandishi: Emmanuel Mbogo

Emmanuel Yakobo Mbogo ni mwandishi wa kazi za fasihi na kazi nyengine za kimaadili, kijamii na kidini. Ni muumini wa dini ya Kikristo, amezaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, huko mkoani Dodoma. Alisoma katika shule ya msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadae alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya Indian (Dodoma Sekondari kwa sasa) na kuhitimu mwaka 1967. Aliwahi kufanya kazi ya ukarani katika Wizara ya Kilimo, mkoani Dodoma kabla ya kupata matokeo yake ya sekondari. Mwaka 1968, alijiunga na Chuo cha cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na kuhitimu mwaka 1969.

Mwaka 1973 alijiunga na masomo ya shahada ya Ualimu na Sanaa za maonyesho katika chuo cha Ualimu Chang’ombe, kilichopo jijini Da-es-Salaam na kuhitimu

mwaka 1974. Baada ya kumaliza mafunzo yake, alipangiwa kufundisha katika chuo cha Ualimu Katoke, ambapo mnamo mwaka 1976, alijiunga na Chuo Kikuu cha Da-es-Salaam, kusomea shahada ya kwanza na ya pili katika Sanaa za Maonyesho (B.A in Theatre Arts na M.A in Theatre Arts). Akiwa chuoni hapo alitunga tamthilia yake *Tone la Mwisho* (1981). Akiwa bado mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Mbogo, alihitimu masomo yake ya shahada ya Sanaa za maonyessho mwaka 1981.

Mwaka 1982 alijiunga na Chuo Kikuu cha Humboldt kilichopo mjini Berlin nchini Ujerumani, kwa masomo ya shahada ya tatu katika sanaa za Maonyesho (PhD in Theatre Arts) na kuhitimu mwaka 1984. Baada ya kumaliza masomo yake alirudi nchini na kufanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), ambapo kwa sasa inatambulikana kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), iliyopo Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam hadi mwaka 1989.

Emmanuel Mbogo, amefundisha Vyuo vikuu mbalimbali barani Afrika kama Chuo Kikuu cha Kenyatta huko nchini Kenya mwaka 2003 hadi mwaka 2006. Baadaye alikwenda nchini Rwanda na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Kigali kwa muda wa mwaka mmoja. Mwaka 2008 alirudi nchini Tanzania na kuendelea kufundisha Chuo kikuu Huria cha Tanzania, ambapo hadi sasa ni Professa chuoni hapo.

Kwa kuzirejelea kazi zake alizoandika ambapo nyingi zina mvuto na mnato na zinaleta furaha, huzuni na kukumbusha historia ya bara letu. Mfano mzuri wa kazi zake katika tamthilia ni kama: *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1980), *Tone la*

*Mwisho* (1980), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Fumo Liongo (2009), Sundiata (2011), Sadaka ya John Okello* (2014), *Wangari Mathaai* (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaan* (2015). Kwa upande wa riwaya ni *Watoto wa Mama N'tilie* (2002), *Vipuli vya figo* (2008), *Siri za Maisha* (2010). Katika utafiti huu tulichagua riwaya yake moja ambayo ni *Watoto wa Mama N'tilie.* Kwa hiyo utafiti huu umejikita katika riwaya hiyo.

## 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie

Riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* ni hadithi inayoelezea hali halisi ya maisha ya Watanzania katika hali duni za maisha zilizogubikwa na wimbi la umasikini. Riwaya hii imewachora watoto wa kimasikini wakikosa haki zao za msingi zikiwemo, elimu, afya, lishe, malezi bora na haki nyenginezo.*Watoto wa Mama N'tilie* ni riwaya iliyosheheni maudhui yanazungukia maisha ya maman'tilie na familia zao, kama sehemu ya walalahoi waishio katika miji na vitongoji mbalimbali hapa nchini. Katika riwaya hii mwandishi ametoa ujumbe mzito ambao jamii haina budi kuutilia maanani kuwaendeleza akina maman'tilie kufuatia umuhimu wao katika kulea na kuandaa watoto wa taifa la kesho.

Katika riwaya hii, muhusika mkuu ni Maman'tilie ambaye amekumbana na vikwazo vingi ikiwa ni pamoja na ulezi mzito wa watoto wake na familia kwa ujumla. Ni riwaya ambayo imegusa hisia za walio wengi wakiwemo kina mama. *Watoto wa Mama N'tilie* ni riwaya inayobainisha misukosuko wanayokumbana nayo kama vile umasikini uliokithiri. Riwaya hii inaonesha kwamba bado kina mama hao wanaendelea kufanya juhudi za kupambana na hali hiyo lakini bado wanaonekana

kuachiwa mzigo mkubwa wa ulezi. Hii ni riwaya isiyowekeka chini kwa sababu ya maudhui yaliyomo ndani yake na uzito wake.

## 4.4 Mbinu za Kisanaa katika Ujenzi wa Dhamira ya Malezi ya Watoto

Mbinu za kisanaa huweza kumtofautisha msanii mmoja na mwengine kwa kutambulisha upekee wa msanii mmoja na mwengine katika uumbaji wa kazi ya sanaa (Jilala 2016). Lengo mahsusi la kwanza lilibainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Lengo hili la kwanza limekwenda sambamba na swali la kwanza lisemalo: Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie?* Mtafiti amechambua mbinu za kisanaa zifuatazo: Mbinu ya Ujenzi wa Mandhari, Mbinu ya Mtindo, Mbinu ya Ujenzi wa Wahusika, na Mbinu ya Matumizi ya Lugha.

### 4.4.1 Mbinu ya Ujenzi Wa Mandhari

Uwepo wa mandhari katika kazi ya riwaya huunda mazingira kwa msomaji, kuibua dhamira kadhaa katika kazi husika kunachangia kuikamilisha kazi hiyo. Mwandishi ametumia mandhari mbalimbali katika kazi yake kama ifatavyo:

#### 4.4.1.1 Shule ya Mapepela

Mwandishi amechora mandhari hii kudhihirisha mahitaji ya mtoto kumuelekeza kimaadili kupitia walimu katika mandhari husika. Mfano mwandishi anasema:

> Ilikuwa saa 10:30. Walimu wa Shule ya Mapepela walikuwa wamewaruhusu wanafunzi warudi nyumbani. Mwalimu Mkuu, Mwalimu Chikoya aliwatangazia wanafunzi: "Wote ambao hamjalipa

> ada na hamna sare. Hakuna shule! Nisizione sura zenu bila ya ada na sare. Waambieni wazazi wenu hivyo" (uk 1)

Tendo hili liliwapelekea watoto wa Maman'tilie wajiingize katika matendo maovu kama wizi, ujambazi na madawa ya kulevya. Mfano wa watoto walioathirika na kadhia hii ni pamoja na: Peter, Zita, Musa, na Dani. Mandhari ya shule imesaida kutuchorea dhamira ya malezi kwa sababu ni mandhari halisia kwa watoto kufunzwa maadili mema. Tabia ya baadhi ya walimu, mfano, mwalimu Chikoya kuwafukuza watoto shule kwa sababu ya kukosa ada na sare ya shule si katika jambo zuri.

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa matukio, unaohusu namna matukio yanavyopatikana katika hadithi, yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya fasihi: Ni kuwa mwandishi ametuchorea visa vilivyofuatana kwa msomaji kupata picha ya kisa cha watoto kufukuzwa shule. Jambo hilo limepelekea watoto kuharibika kimalezi na hatimae kuishia katika mazingira mabaya ikiwemo madawa ya kulevya.

#### 4.4.1.2 Kituo cha Basi

Kituo cha basi cha Msufini, ni pahala walipokutana Peter na Musa ambao ni miongoni mwa watoto walioathirika kwa kufukuzwa shule. Mandhari waliyokutana ni sehemu yenye harakati nyingi kwa watu mbalimbali kama wasafiri, wafanyabiashara na wengineo. Mandhari hii imemsaidia mtafiti kubaini tabia ya Musa kujishirikisha na biashara ya kuuza sigara baada ya kuacha shule kama mwandishi anavyoeleza:

> "…Alikwenda hadi kituo cha basi cha Msufini. Watu walikuwa wengi, wasafiri, wafanyabiashara, wanunuzi, wenye kazi, wezi, watoto kwa wakubwa.…..

> “Nani wewe!” Mtu alikuwa amemgusa begani naye aligeuka. “Aa! Musa.”
> “ Habari zako, Peter”
> “Nzuri Musa,” Peter alijibu. Alimuona Musa kashika paketi za sigara, anauza. “Za nani?”
> Musa alijibu, “Mimi nimeacha shule. Siku hizi napata pesa chungu nzima.” (U.k.17)

Katika nukuu hii, mandhari ya kituo cha daladala (stendi) ni sehemu tata katika malezi ya watoto, kutokana na mazingira ya mchanganyiko wa harakati za watu. Hili linadhihirika pale tunapomuona Musa na harakati zake za kuuza sigireti hali akiwa na umri wa kwenda shule.

Nadharia ya Simiotiki imefanikiwa kuonesha ubunifu katika kazi ya fasihi. Utafiti huu umebaini kuwa kutokana na ubunifu huo wa mtiririko wa visa katika riwaya hii ya *Watoto wa Mama N’tilie*, kufanikisha kuibua dhamira ya malezi ya watoto, kwa kuunda mandhari hatarishi kwa watoto hao na kuwapelekea kuingia katika matendo makubwa kinyume na umri wao. Utafiti huu umebaini kuwa mandhari ya stendi, huwahusisha hasa watoto ambao hufukuzwa shule na hujiingiza katika wimbi la maasi yakiwemo wizi na utumiaji wa madawa ya kulevya.

#### 4.4.1.3 Dampo la Tabata

Katika kutumia mbinu ya mandhari ya dampo la Tabata - jijini Dar-es-Salaam, utafiti huu umebaini mandhari mbalimbali zinazoakisi uhalisia wa jamii yetu. Mandhari hizo zimesaidia kuonyesha dhamira ya malezi ya watoto kwa wale waliokosa malezi mema. Mwandishi anasema:

> “Peter alishika njia. Alitembea kwa muda wa dakika arobaini hadi kukaribia Tabata. Watu wa jiji hili kubwa walikuwa na msemo;

> Ukienda Tabata utapata. Barabara kubwa, nzuri, ya lami, ilikuwa inakwenda kiwanja cha ndege cha Kimataifa. Ilipendeza na kuvutia macho. Ilikuwa ni barabara pana iliyogawanywa kushoto na kulia, katikati milingoti ya taa za stima. Kama ungesafiri usiku kupita barabara hii, ungeona taa hizo zinavyowaka na kumetameta. Lakini uzuri huu ulikuwa karibu sana na takataka za *dampo* la Tabata. (Uk.19)

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa ishara, utafiti huu umebaini kuwa; uwepo wa dampo umeashiria umasikini ulokuwepo, na kimbilio la baadhi ya watoto wa mitaani. Suala la kuwepo kwa watoto wa mitaani wanaolitumia *dampo* kutafuta riziki zao, imedhihirisha dhamira ya malezi mabaya ya watoto hao. Mfano mzuri wa wahusika wa tabia hiyo ni Kurwa na Doto ambao hawakuwa na wazazi na hata walezi wa kuwashughulikia.

### 4.4.1.4 Mtaa wa Kisutu

Umasikini kwa sehemu kubwa ya Watanzania, unachangia uporomokaji wa malezi kwa watoto. Baadhi ya wanajamii wanaendelea kutaabika na kupelekea kukata tamaa juu ya maisha yao kutokana na kushindwa kuzikimu familia zao kiuchumi, kiafya n.k. Utafiti huu amebaini kuwa, umasikini katika mandhari ya Kisutu, umepelekea jamii nyingi za kushindwa kumudu malezi mema ya watoto. Mwandishi anasema:

> Wakati huo Kisutu ilikuwa sehemu ya watu wa hali ya chini sana, katikati ya jiji. Vibanda vyake vya kuta za makuti na mbavu za mbwa viliezekwa madebe ya kutu yaliyochakaa. Madebe au mabati haya yalishikizwa kwa misumari au kukandamizwa kwa mawe au magogo ya miti ili yasipeperushwe kwa upepo. Kama mtu angebahatika kupanda ndege akaangalia picha ya Kisutu, angeona vibanda.Vibanda hivyo vingeonekana kama mchafukoge wa vichuguu vingine vikipumua moshi kwa mapikaji. Vijia na vichochoro na vifereji vya maji machafu vilisukana kuzunguka vibanda vya watu wa makaazi haya. Uozo wa takataka ulileta harufu ukazalisha wadudu na funza. Majani yasiyofekwa yalikuwa maskani ya vijoka na majoka. Maji yaliyosimama yalikuwa zahanati nzuri kwa mbu. wakataga mayai yao

> kwa mamia, kwa hivyo, ugonjwa wa malaria ulikuwa tishio kwa afya, maisha na uhai wa wakaazi wa Kisutu. (Uk 36).

Ukosefu wa lishe bora, afya, malazi bora, elimu n.k kumechangia kubadili malezi ya watoto kijamii na kitaifa. Tukirejelea nadharia ya Simiotiki, mtiririko wa ujenzi wa mandhari umeakisi malezi ya watoto kutokana na mpangilio wa visa namna ulivyofuatana na uhalisia. Katika uhalisia tunaona kuwa hadi baadhi ya maeneo mfano katika jamii ya Watanzania yanaashiria mandhari ya umasikini

#### 4.4.1.5 Dukani kwa Mhindi – Rhemtullah

Athari ya ukosefu wa malezi bora kunasababisha watoto kujiingiza katika wizi. Hili limedhihirika kwa mwandishi kutuchorea mandhari ya dukani kwa Mhindi katika kuibua dhamira ya malezi ya watoto kama ifuatavyo:

> Jiji lilikuwa limeshonana midomo yake yote, midomo ya magari, viwanda, watu hata ndege na kuku wa kufugwa. Dakika tano baadaye sauti ya saa kubwa ya Mnara wa Uhuru ilisikika ikilia ndo, ndo, ndo, ndo, ndo, ndo! Mara sita. Ilikuwa saa 6 usiku. Mtaa wa Nkurumah nao ulikuwa kimya. Nje ya duka la Rhemtullah… Saa 6: 26 hivi Kurwa alistuka na, kwa wepesi wa ajabu, alilala chini kama nyoka, akatulia. Jicho lake moja alilitembeza akifuata mwanga wa gari la polisi lililokuwa katika doria. Lilipita hatua chache karibu yake, likielekea Mnazi mmoja … (Uk.42-43)

Nafasi ya mzazi/mlezi ni kiini cha malezi bora kwa watoto, kinyume cha hayo hupelekea watoto kujiingiza katika tabia mbaya ya wizi, ujambazi na kutokuwa na mwisho mwema, kama kupoteza maisha. Mfano Doto na Dan.

Nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa matukio, imeibua tukio ovu kwa watoto. Kwa mfano, Kurwa na wenzake wakiwa na dhamira ya wizi katika mazingira

hatarishi. Katika utafiti huu, nadharia hii imesaidia kuwaasa watoto, kutojiingiza katika matendo maovu.

#### 4.4.1.6 Nyumbani kwa Maman'tilie

Mandhari nyengine iliyoonyesha dhamira ya malezi ya watoto, ni mandhari ya nyumbani kwa mzee Lomolomo na Maman'tilie. Mwandishi anasema:

> "Hii sebule ilitumika kama chumba cha kulala vilevile. Zita alitandika mkeka sehemu yake, akalala. Naye Peter alitandika sehemu yake, lakini hakulala...akaanza kusoma kwa mwanga hafifu wa koroboi. (uk.9) Aliyatembeza macho yake pale sebuleni; hakuna Peter wala Zita. Alitazama chini, akaona ni pachafu vya kutosha, alitema mate, akayafukia kwa kitifutifu cha udongo...(uk.67).

Nyumbani kwa Mzee Lomolomo, mwandishi amechora picha ya mazingira wanayoishi na kuibua dhamira ya umasikini. Mzee huyu alikuwa ni mlevi na haonekani kujishughulisha na kazi yoyote ya kimaendeleo. Utafiti umebaini kuwa, ukosefu wa mashirikiano na kujituma hurudisha nyuma maendeleo kwa familia.

Katika utafiti huu, nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa matukio, umeakisi muendelezo wa dhamira ya malezi ya watoto. Kupitia nadharia hii, wazazi/walezi wanawajibu wa kusimamia majukumu yao ipasvyo.

#### 4.4.1.7 Kiwanda cha Urafiki

Kiwanda cha Urafiki ni sehemu ya biashara kwa Maman'tilie. Alitumia eneo hilo kuwauzia chakula wafanyakazi wa kiwanda hicho. Mbogo ametuchorea mandhari hii kutuonyesha,mbali ya juhudi za Maman'tilie, bado suala la malezi ya watoto katika familia hii ilikuwa gumu, Mwandishi anasema:

> Pesa alizokuwa anazipata kwa kuuza ugali na maharage kule kiwanda cha Urafiki hazikutosheleza matumizi ya nyumbani, sembuse ada na sare za watoto! Mumewe mzee Lomolomo alikuwa lofa, mtu wa kazi za kijungujiko na vipesa vyake vilivyoishia kwenye pombe za chang'aa au gongo (Uk.7).

Katika nukuu hii, utafiti umebaini, Mwanamke ananafasi mbalimbali katika familia. Mfano, mlezi wa familia, mfanya biashara, mshauri na jirani mwema.Pamoja na hayo hushindwa kuikimu familia, kwasababu 'kidole kimoja hakivunji chawa'.

#### 4.4.1.8 Hospitali ya Muhimbili

Upatikanaji wa huduma ya afya kwa jamii husaidia mzazi/mlezi kumlinda mtoto na magonjwa. Mwandishi anasema:

> Ilikuwa saa kumi na nusu jioni. Mishale ya mionzi ya jua ilikuwa sasa ni butu. Wakati kama huu Hospitali ya Muhimbili watu huwa ni wengi. Watu waliteremka kwenye mabasi mikononi wameshika vibahasha vya chakula, uji, maji ya machungwa, matunda na kadhalika. Walikuwa wanakuja kuwatazama wagonjwa wao, ndugu zao, kaka, dada, mama, baba, shangazi, babu, na watoto wao…. (Uk. 88).
> Maman'tilie na Mama Sara walisimama, wakajiunga na msururu wa watu wengine waliokuja Muhimbili kutazama wagonjwa wao…. Walimaliza ghorofa ya pili na sasa walielekea juu zaidi. Zenabu mbele, Mama Sara nyuma na Maman'tilie katikati. Walipokaribia mlangoni…
> Hamadi!
> Mtume!
> Pazia lile!
> Mioyo ile mitatu ilitumbuka machungu pwaa! (Uk.90)

Umasikini na ukosefu wa elimu ya afya, husababisha vifo visivyotarajiwa. Maman'tilie alichelewa kumpeleka Zita hospitali, alieugua kichaa cha mbwa.Pamoja na kupewa matibabu, alifariki. Utafiti umebaini kuwa, kunawakosesha watoto haki

ya kupata huduma ya afya mapema na husababbisha kifo. Mfano, Zita, baada ya kung'atwa na mbwa.

Nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa matukio, msanii ameunganisha mtiririko wa visa kuibua picha halisi ya dhamira ya malezi ya watoto kupitia huduma za kiafya. Kwa kurejelea nadharia hii, utafiti umeendelea kusisitiza umuhimu wa wazazi kuwaangalia afya za watoto mapema kwa maendeleo yao.

Ni ukweli usiopingika kwamba mandhari katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* imesadifu vyema kuibua dhamira ya malezi kwa watoto na kujenga uhalisia wa mada ya utafiti ipasavyo. Hivyo, dhana ya mandhari imekuwa na nafasi kubwa katika maendeleo ya utafiti huu kwa ujumla.

### 4.4.2 Matumizi ya Mtindo

Mwandishi ametumia mitindo kama; nyimbo, ngoma, michoro, majibizano kufikisha dhamira ya malezi kama ifuatavyo:

#### 4.4.2.1 Nyimbo

Matumizi ya mtindo wa nyimbo umejitokeza katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Mbinu hii imechangia kudhihirisha dhamira ya malezi ya watoto. Mfano, wimbo wa mzee Lomolomo, mwandishi anasema:

> Huyo mlevi aliyeimba wimbo huko nje alimjua sana.Ulikuwa wimbo wa
> mdundiko.
> Kuleni nae
> Hata bangi vuteni nae

> Lakini ni bure
> Mwenzenu nimezaa nae
> Pepepe kijani cha mbaazi
> Kijaluba na msondo
> Kiboko yao (Uk.10).

Mfano mwengine wa nyimbo ya mzee Lomolomo ni:

> Kuleni nae
> Hata bangi vuteni nae
> Lakini ni bure
> Mwenzenu nimezaa nae…(Uk.11).

Utafiti umebaini, nyimbo za kilevi huashiria dhamira ya malezi mabaya. Ni dhahiri kuwa wahenga wanasema: "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Mfano, mtoto Peter baada ya kufukuzwa shule aliathirika kisaikolojia, hatimae kujishirikisha katika biashara ya madawa ya kulevya na kuishia jela (uk 98).

Utafiti umegunduwa kuwa, ukosefu wa ushauri nasaha kwa wazazi na watoto wao, huweza kuwapelekea watoto hao kushindwa kupata maamuzi sahihi. Mfano, Peter kukamatwa na vyombo vya dola na kuishia korokoroni.

Mwandishi ameendelea kututolea wimbo wa mzee Lomolomo kwa wanawe akiwa amelewa . Mwandishi anasema:

> …Mara walisikia sauti ya wimbo. Zita na Peter walicheka. Wimbo ulisema:
> Siwezi kuuwa mtu mama
> Dhambi kwa Mungu mama wee
> Shauri yako, shauri yako wee
> Siwezi kuuwa mtu mama
>
> Dhambi kwa Mungu mama wee
>
> Kurwa aliuliza, "Nani?"
> "Baba," Peter alijibu. "Leo karudi mapema kidogo." Zita alisimama, akafungua mlango. "Shikamoo baba"

> Mzee Lomolomo hakuingia mara moja. Alibaki kasimama pale mlangoni. Aliyumba, uso wake uliopendeza kwa chang'aa aliupeleka mbele… "Wanangu… m-m-mnakula?"
> "Ndiyo, baba."
> "Vizuri. Vizuri sana. Na mama yenu ? "
> "Bado kurudi, baba."
> "…Zita mwanagu, mboga gani leo?"
> "Leo nyama baba." (Uk. 70.)

Kupitia nukuu hii, watoto hupata faraja na kufurahia maisha wanapokuwa na mzazi au wazazi wao pamoja. Jambo hili limedhihirika kwa watoto Zita na Peter baada ya kusikia wimbo kwa baba yao.

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki, kupiptia msimbo wa matukio, unahusu namna matukio yanavyopatikana katika hadithi yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi: Utafiti huu umebaini kuwa ukaribu mzuri wa wazazi kwa watoto hujenga upendo.

Kwa kuendelea zaidi, wimbo wa redioni aliousikia Peter nyumbani kwa Musa umemshawishi kujiingiza katika atarehe, Mwandishi anasema:

> Musa alicheka kwa furaha, akaweka kanda na mara muziki ukaenea pale chumbani. Hivi:
> Juani motooo. Tena ni mwangazaa. Wa duniaa
> Nadina yoo. Nadina yoo Iyooo.Nadina mamaa
> Tuombe Mungu baba. Yoyooo. Atuhurumie dhambi
> Zetu mamaa. "Nani huyoo?" Peter aliuliza.
> Musa alisema,"Humjui! Mbilia Beli huyo! 'Mzairwaa' …sasa unasemaje Peter…? Nikukonekti kwenye mesheni zetu za unga na coca?" (Uk.78).

Mtoto kwa hakika huwa bado anahitaji kuwa mikononi mwa wazazi wake. Tabia hii imehatarisha maisha ya Peter kwa kujiingiza kwenye shinikizo rika na kushawishika

kuingia katika biashara haramu ya madawa ya kulevya kwa tamaa, baada ya kumuona Musa ana busara zisizo kifani. Vilevile baadhi wazazi huwashirikisha watoto wenye umri mdogo kwa maslahi yao binafsi.

Nadharia ya Simiotiki kwa kurejelea nyimbo kadhaa, imeashiria starehe zilizoibua tamaa mbaya. Hivyo, msimbo wa ishara uliotumika umesaidia katika utafiti huu, kuwazindua watoto wasijiingize katika tabia hizo mbaya. Kwa upande wa wazazi wasimamie vyema majukumu ya ulezi wa watoto wao.

### 4.4.2.2 Ngoma

Mtindo wa aina hii ni mfano mwengine wa kuibua dhamira ya malezi ya watoto. Mfano, umasikini umechangia ukosefu wa malezi mema kwa watoto na jamii kujishirikisha zaidi katika anasa kuliko harakati za kiuchumi. Mwandishi anasema;

> Mara huko mtaani akasikia ngoma ya mdundiko ikipita,
> Wamooo Eee! Wamooo! Eee!
> NGOMA: Ndi-ndi-ndi! Ndi-ndi-ndi
> WIMBO:Mume wako sikumwita.Kanisimamisha
> Mwenyewe.Kaiona dizaini na
> Hii shepu yenyewe.
>
> Mtaa wa Manzese
> Kuna mgome-mgome
> Na huo umbea wenu
> Shoga yangu mkome
>
> Nipeni shilingi yangu
> Nikanunue kibwaya
> Ninasimangiwa kula
> Kula kwenyewe kwa kaya.
> Umasikini mbaya
> Tena unatia haya
> Ningelikuwa tajiri
> Mbona ningegaragara.

> Peter hakuufuata ule msururu wa mdundiko. Alibaki palepale nje akiwatazama watoto na wanawake wanavyotimua vumbi. Masikio na akili yake ilinasa ule ubeti wa mwisho, uliohusu umasikini na utajiri. (Uk.16)


Nukuu hii inathibitisha kwamba, baadhi ya wazazi wanatabia kutojishuhulisha na harakati za kiuchumi badala yake kupenda starehe zaidi. Data zimedhihirisha kuwa, ya wanawake ndio wajenzi wa familia bora, lakini baadhi yao ndio wabomowaji wa familia hizo. Mfano, Peter hakuufuata msururu wa ngoma alibaki pale nje akiwatazama watoto na wanawake wanavyotimua vumbi' (uk.16).

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki msimbo wa ishara, imedhihirisha kuwa, matumizi ya ngoma yanaashiria maisha ya wanajamii jinsi yalivyo.Nadharia hii imekuwa msaada mkubwa katika utafiti huu kwa kuizindua jamii kusimamia malezi bora na matumizi bora ya wakati.

#### 4.4.2.3 Michoro

Matumizi ya michoro pia yamebainika katika utafiti huu kupitia kipengele cha mtindo**.** Mwandishi ametumia mtindo wa michoro kufikisha dhamira ya malezi ya watoto. Michoro huwavutia watoto katika usomaji wa matini.

**Watoto wa Shule kurudi Nyumbani:** Mwandishi ametuonyesha mchoro wa watoto wa shule wanaorudi nyumbani baada ya kufukuzwa na mwalimu Chikoya. Mchoro huo unaonyesha Zita anatafunwa na mbwa na huku wenziwe wanamkimbia mbwa huyo kama kielelezo kinavyoonyesha hapo chini. (uk.3):




**Mchoro nambari 1: Data kutoka riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Julai 2017**

Katika data zilizokusanywa, utafiti huu umebaini kuwa uwasilishaji wa mchoro huu umeibua dhana ya uzembe na udhalilishaji ulikofanywa na Mwalimu Chikoya kuwafukuza watoto shule na kumesababisha mtoto Zita kutafunwa na mbwa.

Nadharia ya Simiotiki kupitia utafiti huu, umebaini baadhi ya wazazi huchelewesha huduma ya afya kwa watoto wao, jambo ambalo hupelekea madhara


**Dampo la Tabata:** Mchoro mwengine unaonesha Doto, Kurwa na Peter wako katika *dampo* la Tabata. Doto anagombana na Peter (Uk.20). Dhamira ya malezi mabaya ya watoto imeibuka kupitia mazingira waliyopo watoto hawa. Watoto hawa wamekuwa ni watoto wa mitaani wanaojitegemea kimaisha. Peter alikwenda jaani (dampo) kutafuta njia mbadala ya kupata mtaji katika biashara ya mama yake ya kuuza chakula gengeni ili apate kurudi shule.




**Mchoro nambari 2: Data kutoka riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Julai, 2017**

Watoto wakikosa malezi na huduma kutoka kwa wazazi wao hukomaa haraka kiakili na kutafuta njia ya mkato ya kutafuta riziki zao. Hufanya hivyo bila ya kuchukua hadhari yoyote.Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa ishara, imekuwa na mchango muhimu katika utafiti huu kuishauri serikali kuzidi kutoa elimu ya malezi mema kwa jamii. ili kuibua vipaji endelevu kwa watoto.

**Nyumbani kwa akina Kurwa:** Michoro inajenga dhamira ya haraka kwa msomaji, mchoro wa hapo chini unawakilisha dhamira ya malezi ya watoto. Unaoonyesha nyumbani kwa akina Kurwa akiwa na mazingira duni, nyumba mbovu amekaa nje, nguo yake inaviraka, huku njiani anamtazama mama mmoja akipita huku akiwa na watoto wake wawili, mvulana kama miaka saba, na msichana takriban miaka mitano, wakiwa na furaha huku wanatembea wakielekea dukani (uk.39).



**Mchoro nambari 3: Data kutoka riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Julai, 2017**

Katika mchoro huu mtafiti amebaini kuwa Kurwa ameathirika kisaikolojia, kwa kukosa upendo kwa wazazi, malezi bora, elimu n.k.. Mtafiti anashauri kuwa,

wazazi/jamii kujenga moyo wa huruma kuwasaidia watoto wa aina zote hasa, wenye kuishi katika mazingira magumu. Mfano Mama Zita alikubali kuishi na Kurwa baada ya kuletewa nyumbani na Peter. Mtafiti anaamini kwamba mzazi ni mmoja lakini walezi ni wengi.

**Ugomvi:** Mchoro mwengine ulioonyeshwa na mwandishi ni baada ya Peter kuelekea dukani kununua dawa kwa ajili ya kumtibu Kurwa. Ghafla Zita alishindwa kustahamili na mara wakaanza kupigana miereka nje, kundi la watu wanawashangiria! (Uk.62).



**Mchoro nambari 4: Data kutoka riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Julai 2017**

Mtafiti amebaini tabia ya wanajamii kwa nyakati za sasa kukosa mashirikianao ya malezi ni jambo la kawaida, tabia ya kupigana kwa watoto ni tabia mbaya lakini

jamii walishangilia pasipo kujali. Mtafiti anashauri kuwa, viongozi wa dini, siasa na taasisi nyengine ndani ya jamii husika wawajibike kukemea wazazi/jamii zenye tabia hizi.

#### 4.4.2.4 Majibizano

Mtindo huu huvuta umakini zaidi kwa msomaji na pia hupelekea kukazia dhamira aliyoikusudia mwandishi. Mfano mzuri unaodhihirisha mtindo huu ni majibizano baina ya mama Zita (maman'tilie) na mtoto wake Zita. Hii imejitokeza wakati wa maandalizi ya kupika chakula. Mwandishi anaeleza kupitia wahusika hao kama ifuatavyo:

> "Mama aliita, Zita wee!"
> "Bee mama"
> "Ebu washa jiko, tupike"
> "Ndiyo mama." (uk.7)

Mtafiti amebaini kuwa mwandishi ametuonyesha umuhimu wa malezi mema ambayo mzee anatakiwa awenayo kwa mtoto hasa wa kike. Watoto wa kike kwa hakika wanatakiwa kuwa karibu na mama zao. Mtafiti amebaini kuwa mama hupenda kumuelekeza binti yake akiwa ni mwenza wake wanapokuwa pamoja nyumbani. Mtafiti anashauri kuwa mama awashirikishe watoto wa jinsia zote katika kazi za nyumbani.

Dondoo nyengine yenye mtindo wa majibizano ni pale Maman'tilie alipomuhoji mwanawe Zita baada ya kurudi shuleni kama ifuatavyo:

> "Shikamoo mama… Mama Shikamoo." Maman'tilie alimtupia jicho bintiye Zita akasema, "Na hiyo nguo vipi ?" "Kwani vipi mama?"

> “Vipi namna gani?” Maman’tilie alisema huku mkono wake mmoja umeshikilia sufuria chafu.
> “Mbona chafu hivyo na leo ndio kwanza Jumanne”“Mbwa mama! Karibu yule mbwa amg’ate.”Zita akasema,” Amenikwaruza kidogo na makucha yake.” Aligeuza mguu wake ili kumuonyesha mama yake. Maman’tilie alitoa macho kidogo akaangalia kale kijikwaruzo kadogo na vijidamu ambavyo sasa vilikuwa vimekwishakauka. Mama alisema,“Msiwe mnacheza na kuchokoza mbwa, ala!” “Hata mama!” Peter alisema.“Sisi tulikuwa tunapita tu, akaanza kutufukuza.” “Nendeni, mbadilishe nguo za shule,” “Hee! Mama? ”Zita alianza.“Hizi si nguo za shule mama” (Uk.6)

Mwandishi ametumia mtindo wa majibizano kufikisha dhamira ya malezi kwa watoto. Katika nukuu hii, mtafiti amebaini kuwa mtindo wa majibizano umeisaidia hadhira kuvutika na usomaji wa riwaya hii pasi na kuchoka.

Mtafiti anawashauri wazazi/walezi, waalimu na jamii kwa ujumla kujenga urafiki na ukaribu kwa watoto. Wazazi na walimu watakapojenga urafiki watawaondolea woga na kuwafanya waweze kujenga ujasiri na moyo wa kujieleza pale wanapofikwa na majanga mbalimbali.

### 4.4.3 Mbinu ya Ujenzi wa Wahusika

Mwandishi katika riwaya yake ya *Watoto wa Mama N’tilie*, ametumia wahusika kwa lengo la kufikisha dhamira ya malezi. Wahusika aliowabuni katika kazi hii ni: Peter, Zita, Zenabu, Lomolomo, Maman’tilie, Kurwa, Doto, Dan, Mama Sara, Sara, Polisi, Master Baron, n.k Mwandishi amewachora wahusika wake kwa mujibu wa nafasi zao katika riwaya hii kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.1 Maman'tilie

Maman'tilie ni mke wa mzee Lomolomo mwenye mapenzi mema na mumewe, ana watoto wawili, Peter Lomolomo na Zita Lomolomo. Mtafiti amebaini kuwa ni mama anaependa kujituma katika harakati za kiuchumi ili kukidhi mahitaji ya lazima kwa familia yake, pamoja na kuwapatia ada na sare watoto wake kwa lengo la kurudi shuleni. Ukwamishaji wa harakati za kiuchumi kwa watu masikini hukwamisha juhudi zao,suala kama rusha ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii. Familia nyingi za kimasikini hujikuta kushindwa kukidhi mahitaji ya watoto kama elimu,afya n.k. Maman'tilie ni mama mwenye huruma kwa watoto mfano alimpokea Kurwa na kuishi nae kama mtoto wake, pamoja na halingumu ya maisha inayomkabili (uk75). Kwa kuyadhihirisha haya mwandishi anasema:

> Saa mbili usiku ugali na maharage ulikuwa tayari. Maman'tilie na wanawe wawili walikaa, wakala, wakanywa maji, wakamshukuru Mungu. Jikoni walikuwa wamembakizia Lomolomo, mzee wa nyumba au mzee wa maji, kama walivyomwita wakati mwengine. (Uk.7)

Katika nukuu hii mtafiti amebaini kuwa nafasi ya mwanamke akiwa kama mama wa familia mwenye jukumu la kutayarisha chakula na kuwafundisha watoto malezi mema kama adabu za kula ni miongoni mwa maadili katika familia. Pia mwanamke huwa ni mke mwema na matunzo kwa mume, Mtafiti kupitia data alizokusanya amebaini kuwa ukosefu wa mashirikiano katika familia hasa katika majukumu ya malezi ya watoto huathiri watoto na kukosa muelekeo mwema wa maisha. Mtafiti anashauri kuwa wanawake wapewe kipaumbele katika kupata elimu na kupewa mikopo ya kuanzisha biashara zao ndogondogo. Hali hii itawawezesha wanawake

hao kujiajiri na kupunguza mzigo mkubwa kwa taifa na kujenga mustakbali mwema kwa watoto kwani wanawake ni kiungo muhimu kwa jamii na taifa kwa ujumla.

#### 4.4.3.2 Lomolomo

Ni mume wa Mamantilie, mwenye watoto wawili, hana malezi bora kwa wanawe. Mzee Lomolomo ana kazi ya kijungujiko tangu apunguzwe kazi Bandarini. Pia mlevi na mvivu asiyeijali familia yake. Kwa kulithibitisha hili mwandishi anasema:

> Pesa alizokuwa anazipata kwa kuuza ugali na maharage kule Kiwanda cha Urafiki hazikutosheleza matumizi ya nyumbani, sembuse ada na sare ya watoto! Mumewe mzee Lomolomo alikuwa lofa, mtu wa kazi za kijungujiko na vipesa vyake vilivyoishia kwenye pombe za chang'aa au gongo (Uk.7).

Mtafiti ambaini kuwa mara nyingi baadhi ya mwanamme huwa kikwazo katika maendeleo ya familia, kwa kutumia muda mwingi katika anasa (pombe) na kuwakosesha watoto haki ya kupata elimu, haki ya kupata huduma za afya, haki ya kusikilizwa, haki ya kupata lishe na malazi bora, n.k. Vilevile mwandishi anasema:

> Mzee Lomolomo aliamka, zile kelele za Wuu! Wuu! za binti yake hatimaye kupelekwa hospitali hakuwa na habari nazo. Alisimama toka kitandani kwa unyonge. Jana alipotoka ulevini alijitupa kitandani hivyohivyo na nguo zake. Alipepesuka kwa njaa. Sehemu zote za viungo vya mwili zilikuwa zinatetemeka. Maradhi haya ya kutetemeka yalisababishwa na chang'aa. Na dawa ya kuutibu ugonjwa huu, Lomolomo alisema, ni kupiga mzinga wa chang'aa kila siku. Lomolomo alikuwa anasikia njaa"…Leo nitaitafuta hazina yao,"mzee Lomolomo alijisemea. Alijua kuwa Maman'tilie na wanawe walikuwa na akiba ya fedha iliyofichwa mle ndani ili baadae walipe ada ya shule. Alianza kazi…." (Uk.86)

Mtafiti kupitia ukusanyaji wa data zake amebaini kwamba ulevi wa kupindukia unaiua familia, jamii na taifa kwa ujumla kwa kulikosesha nguvu kazi ya sasa na

baadaye. Pia mtafiti amebaini kuwa mashirikiano ndani ya familia ni silaha njema kwa wapendanao, ni baraka kwa kizazi katika kuwapa watoto malezi mema.

Mtafiti anashauri kuwa wazazi waepuke tabia ya ulevi na badala yake washirikiane katika nyanja za kiuchumi, malezi, elimu, afya n.k ndio silaha bora ya mafanikio katika malezi ya watoto na taifa pia.

**4.4.3.3 Peter na Zita**

Peter na Zita ni watoto wa mzee Lomolomo na Mamant'ilie, ni wanafunzi waliofukuzwa katika shule ya msingi ya Mapepela, kwa kutolipia ada na kukosa kuvaa sare ya shule. Watoto hawa walikuwa kati ya umri wa miaka 12.

Mtafiti kupitia ndugu hawa amebaini kuwa ni wenye mapenzi ya dhati baina yao na kwa wazazi wao, wote walikuwa na bidii ya kazi kwa lengo la kutaka kurudi tena shule. Zita aliugua ugonjwa wa kichaa cha mbwa na kufariki dunia, Peter aliishia kukamatwa na askari wa jeshi la polisi kwa kushiriki kuuza madawa ya kulevya (Uk.98), baada ya kukosa mwelekeo wa kurudi shule na kukosa kupata ushauri mwema hasa kutoka kwa baba yake mzazi.

Katika kufikisha dhamira ya malezi ya watoto, mtafiti ameona nafasi ya wahusika watoto katika kufikisha ujumbe kwa jamii ya watanzania na dunia kwa ujumla, hususan nchi za Kiafrika, ambapo suala la ulezi wa watoto hukabiliwa na changamoto kadhaa mfano; vita vya wenyewe kwa wenyewe, maradhi sugu mfano Ukimwi na kipindupindu, ulevi na uvivu, ukosefu wa ajira, njaa n.k. huwakosesha

watoto hao haki zao za msingi kama: elimu, afya, lishe, malazi n.k. hatimae watoto hao huishia kupata magonjwa, kusekwa magerezani na mwisho kufariki dunia.

#### 4.4.3.4 Doto na Kurwa

Doto na Kurwa ni watoto mapacha wa mzazi mmoja (mama) ambae alifariki baada ya kuugua malaria (Uk.36) tendo lilowapelekea kulelewa na rafiki wa mama yao (Jane) ambae kwa bahati mbaya nae alifariki dunia kwa ajali ya gari (Uk.37), hatimae watoto walijikuta kuwa ni watoto wa mitaani kwa kukosa mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ukiwemo upendo kutoka kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla hasa baada ya kufukuzwa shule kwa kukosa ada na sare.

Doto na Dan wanafariki dunia baada ya kuiba dukani kwa muhindi na kushambuliwa kwa risasi na mlinzi. Kurwa aliishia mikononi mwa Maman'tilie na kulelewa huko.
Mtafiti amebaini kuwa, watoto hawa wamechorwa na mwandishi kuwakilisha kundi kubwa la watoto wa mitaani nchini, wanaokosa malezi aidha kwa kuwa na mzazi mmoja, kufiliwa na wazazi, kukosa jamaa wa kuwalea halkadhalika wazazi kukabiliwa na umasikini mwishowe kuwaacha watoto kujichumia wenyewe na hatimae kuishia kuwa machokoraa jambo linalowakosesha kupata malezi na haki zao za msingi.

#### 4.4.3.5 Zenabu

Zenabu ni mfanyakazi wa klabu iliyoitwa *Kikale Bar*, ni jirani mwema wa Maman'tilie, mwenye mashirikiano, huruma na mapenzi ya dhati kwa watoto. Zenabu na Mama Zita (Mamantilie) walipendana sana na kushirikiana vyema katika malezi ya watoto Peter na Zita, kwa mfano mwandishi anasema:

> Zenabu aligeuka,"Njoo unawe."Alimpeleka Peter uani, akampa maji. Peter alinawa uso akarudi chumbani, "Kaa". Peter alikaa kwenye kiti maji bado yanamvuja usoni. Zenabu alimmiminia chai ya rangi kwenye kikombe cha plastiki. "Haya, kunywa!" Peter hakuichukua chai ile mara. Badala yake aliikausha mikono yake kwenye kaptura. Macho yake yalimwangalia Zenabu akipakua sahani ya muhogo. Alimwekea mezani. "Kula uende kucheza." (Uk.14-15.)

Katika nukuu hii, mtafiti amebaini kwamba si kawaida kwa mwanamke kuwa na tabia au hulka mbaya kwa watoto, ni maumbile yake kuwapenda na kuwahurumia, kuwajali, kuwalea n.k. Hivyo wapo baadhi ya wanawake wenye mioyo ya upendo hata kama watoto hao sio wao. Jamii bora hujengwa na wahusika bora kama Zenabu. Kwani jitihada zake zote zilizidi kujenga mapenzi, ukaribu na ushirikiano mwema wakati wa raha na shida mfano baada ya Zita kuugua na kufariki Zainabu na amama Sara walisimama kidete kumsaidia Mama Zita.

### 4.4.4 Mbinu ya matumizi ya Lugha

Utafiti huu katika kukusanya data za mbinu ya matumizi ya lugha, mtafiti ametumia vipengele vichache kuvichambua ili kufikia lengo la utafiti huu, ambavyo ni tamathali za usemi, nahau, methali, takriri, mjalizo, mdokezo na nidaa.

#### 4.4.4.1 Tamathali za Usemi

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana moja kwa kutumia dhana nyengine tofauti au zinazofanana nazo ambazo hutumiwa kwa lengo la kupanua , kupuuza, kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwa hadhira. (Jilala, 2016). Tamathali za usemi hutumiwa kueleza fungu la maneno, au hata neno, ambalo limegeuzwa maana yake ya

kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyengine. (Wamitila, 2003). Tamathali za usemi zilizotumiwa na mwandishi ni kama zifuatazo:

#### 4.4.4.1.1 Tashibiha

Tashibiha ni usemi unaolinganisha vitu viwili halisi vinavyoonekana, ambavyo vinaleta mshabaha. (Khatibu,1986). Maneno yatumikayo ni: sawasawa na, mithili ya, kama, mfano wa, hutumiwa kufananisha vitu viwili. Msanii katika riwaya yake teule ametumia tashibiha ili kuibua dhamira yake ya malezi kwa kusema:

> Lakini Lomolomo hakumsikiliza, aliendelea kuimba. *Mdomo wake uliokaa kama bakuli la pombe*, ulitamka maneno kwa taabu. (Uk.10)

Katika dondoo hii mwandishi amefananisha mdomo wa mzee Lomolomo na bakuli. Kwa lugha ya kawaida bakuli ni chombo cha kutilia chakula. Mwandishi ametumia neno bakuli kulifananisha na mdomo. Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa Kiseme unaotoa fursa kwa mtafiti kueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi kuchora dhana moja kwenye mazingira ya kawaida na kutumia dhana hiyo kisanii kama ambapo picha ya bakuli imefananishwa au imenasibishwa na mdomo wa Mzee Lomolomo.

Mbogo anaendelea kutumia tashbiha katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* kama ifuatavyo:

> Safari hii mate yenye harufu ya gongo yalitoka kama cheche za moto yakatua juu ya uso wa Maman'tilie. Katika kustuka na hasira, Maman'tilie alimwachilia mumewe, akaanguka chini kama mzigo. Na bado … mwanakwenda we! Puuu!
> Maman'tilie aliruka kama kapigwa na radi. (Uk.12)

Mtafiti amebaini jinsi Mamantilie alivyokuwa anampeleka mumewe ndani akiwa amelewa huku anaongea. Kitendo cha mate yalimtoka na kumuingia mkewe usoni, mate hayo jinsi yalivyotoka yalifananishwa na cheche za moto. Hii ina maana kuwa kitendo hicho kilimkasirisha Maman’tilie “…alimwachilia mumewe akaanguka chini kama mzigo” Mtafiti amegundua matumizi ya lugha ya ishara ikielezea namna mtu anavyopata hasira kubwa kutokana na maudhi aliyofanyiwa mithili ya cheche za moto, na kusababisha kumuwacha aanguke chini. Mtafiti anaona kuwa, mtu mwenye hasira anaweza kufanya jambo lolote hatarishi bila ya kujali madhara yatakayotokea kwake na kwa mtu mwengine.

Mwandishi ameendeleza ubunifu wake katika matumizi ya tashibiha ili kutimiza ujumbe kufika kwa hadhira yake. Katika kulithibitisha hili mwandishi anasema:

Sasa Musa alitoa majani ya mirungi kutoka mfukoni. Aliyatazama kidogo, kisha **akaanza kuyatafuna kama mbuzi**. (Uk.18).

Katika nukuu hii mtafiti amebaini tabia mbaya ya mhusika Musa kutafuna mirungi, jambo ambalo amelizowea kiasi ambacho kwake kuyatafuna haikuwa shida. Mwandishi amaetumia lugha ya picha kuonyesha watoto wanaokosa malezi ya wazazi wanavyoharibika kwa kujiingiza katika matumizi ya mihadharati. Ni ishara kuwa mtoto anaekosa malezi bora huathirika kisaikolojia.

Kwa kuzingatia nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiishara unaohusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihi, mtafiti amebaini kuwa dhana ya kutafuna majani ya mirungi kama mbuzi

imekwenda sambamba na tabia ya baadhi ya wahusika wakiwemo watoto kujiingiza katika matumizi mabaya ya madawa ya kulevya baada ya kukosa malezi bora kutoka kwa wazazi na familia. Hatima ya watoto kama hao ni kukamatwa na vyombo vya dola.

#### 4.4.4.1.2 Tashihisi

Kahigi (1995), Tashihisi ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai. Tashihisi ni tamathali za usemi ambapo vitu visivyo na uhai na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo (Jilala, 2016). Maelezo ya watalamu hawa yanasadifu na ubunifu wa Mbogo katika matumizi ya lugha kwenye riwaya yake ya *Watoto wa Mama N'tilie,* kwamba hapana shaka ni mahiri katika kuibua dhamira zake kwa hadhira na kuteka hisia za wasomaji wa riwaya hii kiasi ambacho hakumchoshi msomaji kuendelea kuisoma kazi yake. Haya yanathibitishwa na mwandishi kwa kusema:

**Moshi mweusi wenye harufu ya kuudhi ulielea hewani na kumlaki mtoto Peter**. Naye Peter aliitikia salamu hizo za ukarimu huku akipiga chafya …(Uk.19).

Mtafiti ameona kitendo cha kulakiana kufanywa na moshi, tendo hili lilimpata Peter alipokwenda dampo kwa ajili ya kutafuta chakula. Vilevile msanii amebainisha namna gani Peter alivyoitikia salamu kwa kupiga chafya.

Mtafiti amebaini kuwa moshi umepewa sifa ya mwanadamu ya "kumlaki" Peter jaani kwa maana ya kuingiwa na moshi mwingi mchafu wa jaani na kushikwa na kikohozi

kikubwa. Kwa kurejelea nadharia ya Semiotiki kupitia msimbo wa kiishara umetumika kutuonyesha namna gani madhara ya moshi wa *dampo* kwa viumbe wakiwemo watoto unavyoleta athari ikiwa ni pamoja na kupata maradhi ya kifua. Kimsingi tashihisi imetumika kwa lengo la kumfanya msomaji ajiulize maswali kwamba kwenda dampo kwa Peter ndiko kulikompelekea kusalimiwa na moshi au dhana hiyo inaashiria suala zima la kukosa malezi na matuzo bora kwa watoto kunakochangiwa na kukosekana kwa mashirikiano baina ya wazazi au walezi wa pande zote mbili (baba na mama)? Bila shaka malezi mema ya pande zote mbili yatasaidia sana kuwakinga watoto dhidi ya majanga kama hayo, yakiwemo ya kwenda kuhangaika jalalani na kusababisha maradhi kwao ikiwemo kifua na hata mangonjwa mengineyo nyemelezi.

Sambamba na hayo mwandishi ameendelea kututolea mfano mwengine wa tashhisi kama ifuatavyo:

**Paa, madirisha na milango ya vibanda vile vilivuta hewa** ile chafu. Mapafu ya wakazi yaliendelea kuteketea kwa moshi,.. (Uk.27).

Mwandishi ametumia tashihisi kuonyesha namna ambavyo hali ya makaazi ya watu masikini ilivyo, mbinu hii imefikisha ujumbe wa dhamira ya malezi ya watoto jinsi yanavyoathiriwa na umasikini, kiasi ambacho moshi wa *dampo* unaingia ndani ya vibanda vyao bila ya shida hali ambayo si maisha mazuri kwa binadamu, kwani vibanda havina sifa ya kuvuta hewa, ila viumbe vyenye uhai ndivyo vyenye sifa hiyo. Ni wazi kuwa msomaji huvutika na kujenga hamu ya kujua kinachoendelea kwa jamii dhidi ya malezi ya watoto katika mazingira hayo.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara unaohusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihi, ambapo dhana ya vibanda waishivyo binadamu kuvuta hewa vimechorwa na mwandishi kujenga picha ya umasikini na vibanda hivyo kupewa sifa ya kupumua kuonyesha hali ya ubovu.

Mbogo, anaendelea kutumia tamathali ya usemi huu wa tashihisi, kwa lengo la kusukuma mbele dhamira iliyojitokeza katika riwaya hii kwa kuipatia hadhira ujumbe uliokusudiwa. Maelezo haya yanathibitishwa na mwandishi kupitia nukuu ifuatayo:

Tena macho yake yalitua juu ya **gunia lile la mchele, lilokuwa limejipweteka** kati ya miguu yao. “Vipi?”… (Uk.30).

Kwa kawaida gunia halina uwezo wa kujipweteka kama binadamu afanyavyo, kujipweteka ni kitendo cha mtu kukaa chini, mwandishi ametuchorea picha ya gunia la mchele wa jaani lakini halikujaa na kuwekwa katikati ya miguu ya Zenabu. Mbinu hii imemithilishwa na nadharia ya Simiotiki kurejelea msimbo wa kiishara, kutuonyesha jitihada ya Peter kutafuta njia ya kuendeleza biashara ya genge la kuuzia chakula  kwa lengo la  kupata kipato ili aweze kurudi  shuleni.

Mbogo aliendelea kudhihirisha kipaji chake cha sanaa na kutilia maanani matumizi ya lugha ya kitamathali ambayo ni tashhisi kama ifuatavyo:

Yalikuwa majonzi makubwa kwa Kurwa na Doto. Wakiwa na miaka minane tu, **makucha ya dunia yaliwatazama bila ya huruma**: njaa, malezi, maradhi na nini sijui! (Uk. 37).

Kwa hakika, mwandishi ameonyesha hali halisi ya watoto hawa, baada ya kuondokewa na walezi wao na kuachwa pweke, hivyo mwandishi ameipa sifa dunia na kuifanya kuwa na sifa ya binadamu kuwa na makucha na kutazama, hali hii imewapelekea watoto Kurwa na Doto kuwa na maisha ya dhiki, huku wakiandamwa na njaa, malezi, n.k. Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki, kupitia msimbo wa matukio: Msimbo huu unahusu namna matukio yanavyopatikana katika hadithi yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi, kunamchorea picha msomaji kuelewa ni tukio gani litakalowakumba watoto hao kutokana na usemi huu wa makucha ya dunia kuwatazama bila ya huruma. Mifano mengine ya tashhisi ni (uk 51, 57, 67, 70 na 90).

#### 4.4.4.1.3 Sitiari

Kahigi (1995) akinukuliwa na Jilala (2016) anasema kuwa sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Sitiari kama tamathali nyengine za usemi, hulinganisha vitu vya aina mbili au zaidi vyenye sifa tofauti na haitumii maneno ya viungo kama vile: mithili ya, kama, mfano wa n.k. Naye Msokile (1992) anatoa maelezo kuhusu sitiari na kusema kwamba, ni tamathali ya usemi ambayo kwa kawaida inahusianisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti.

Matumizi ya sitiari katika kazi za fasihi huipa uhai lugha jinsi inavyotumika katika mazingira maalumu na kuleta maana maalumu. Kwa maana hiyo, tamathali ya usemi ya sitiari katika kazi ya fasihi, riwaya ikiwemo ni mbinu ya kisanaa ambayo msanii anaitumia katika kunasa hisia za wasomaji na kuleta vionjo kwa hadhira na kuipamba kazi zao kwa lengo maalumu katika kusaidia kusukuma mbele dhamira zilizojitokeza kwenye kazi zao.

Mwandishi wa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* ni miongoni mwa waandishi wa kazi za fasihi mwenye ubobezi katika kujenga dhamira mbalimbali kwa hadhira yake kwa kutumia tamathali za usemi. Kwa lengo la kulidhihirisha hilo mwandishi katika riwaya yake ametumia sitiari kama ifuatavyo:

Sasa alipiga mlango ule wa bati teke paa, "Fu-ngu-waa! **Nyama nyie!"** (Uk.10).

Mwandishi katumia lugha ya kulinganisha au kufananisha nyama na binadamu. Tukirejelea nadharia ya Simiotiki, katika msimbo wa ki-seme ambao huu hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi, mwandishi alichora picha ya mnyama kumfananisha na binadamu. Kawaida neno nyama ni ufupisho wa neno mnyama, kwa hiyo binadamu amefananishwa na mnyama.

Mwandishi ametumia sitiari kumchora mhusika wake na tabia yake ya ulevi na kuibua dhamira ya malezi ya watoto kwa wazazi walevi na wazembe wasiokuwa na

utu ndani ya familia zao. Mtafiti anashauri wazazi na walezi kuachana na tabia mbaya na badala yake wazipende familia zao kwa kushirikiana katika malezi.

Mwandishi anaendelea kutumia sitiari katika kusukuma mbele dhamira alizokusudia kama ifuatavyo:

“Marahaba” Sasa macho yake yalituwa juu ya uso wa Kurwa. Alimtazama kitambo **akili inapiga mbizi katika bwawa la pombe.** (Uk.71).

Kwa mnasaba wa hayo, mwandishi hakutaka kutumia lugha ya kulinganisha au kufananisha akili na kitu kingine bali alichora hii sitiari na kile alichokiona katika akili kwamba kupiga mbizi katika bwawa la pombe. Kwa lugha ya kawaida, akili huwanazo binadamu na kwa sababu mhusika alikuwa amelewa, fikira au mawazo yake nayo yalikuwa ni ya kilevi kiasi cha mawazo yake kuelea. Mwandishi anaitaka jamii kuwacha ulevi wa moja kwa moja kwa sababu ulevi hurejesha nyuma maendeleo ya familia ikiwemo malezi ya watoto na taifa kwa ujumla.

#### 4.4.4.2 Tanakali

Senkoro (1982), Tanakali sauti au Onomatopia ni matumizi ya neno ambalo likitamkwa huelekea kutoa maana. Matumizi ya tanakali sauti, hutumiwa na mwandishi katika kuibua dhamira zake kwa hadhira husika. Mbogo hakuwa nyuma katika kazi yake ambapo ametumia tanakali sauti kama ifuatavyo:

Alipinda mgongo kwa mbele, akausikia unalia **ka-ka-ka-kaa!** Alitema mate tena**, phuuuu!** na kuingia ndani.(Uk.5)

Katika kutilia mkazo dhana ya hii ya tanakali sauti, mwandishi ameweza kuonyesha hali ya maradhi yalivyomsumbua Maman'tilie. Matumizi ya tanakali sauti yametumika kutuonyesha namna na hali aliyokuwa nayo Maman'tilie ya maradhi, lakini hakuweza kupumzika bali aliendelea na kazi zake za nyumbani. Mtafiti amebaini kuwa tanakali sauti zimetumika kwenye mazingira ya ugonjwa na sauti ya mgongo kusikika kulia, pia sauti ya utemaji wa mate kusikika, hivyo mwandishi amefanikiwa kutumia usanii wake kwa lengo la kuadhimisha dhamira ya malezi kwa hadhira/wasomaji.

Nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa ishara unaohusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi ya fasihi, msomaji anapata picha ya mtu alieinama na kusikia sauti ya mlio wa mgongo, hivyo kufahamu hali aliyokuwa nayo mhusika tajwa. Vilevile mwandishi ametumia tanakali sauti kuhudhurisha hali ilivyo kwa mhusika wake kama ifuatvyo:

"Niache we mwanamke! Unanishikashika unadhani mimi nimelewa!" Alikohoa **ukho! okhoo!** (Uk.11).

Mwandishi ametumia tanakali sauti kwa lengo la kuonyesha wasomaji tabia mbaya aliyokuwa nayo mzee Lomolomo pamoja na hayo anasaidiwa na mkewe kuingia ndani ingawa anakataa. Pia mwandishi anaendelea kutuonyesha tanakali sauti kwa kusema :

Naye Peter aliitikia salamu hizo za ukarimu kwa kupiga chafya mbili au tatu: **Tcha! Tcha! Tcha!** (Uk.19).

Katika nukuu hii mwandishi ameonyesha hali iliyompata mhusika wake alipokuwa kwenye dampo na jinsi hali ya hewa ilivyomsumbua ambayo ni moshi wa harufu mbaya wa takataka za dampo. Mwandishi ametuonyesha dhamira ya malezi kwa watoto wa mitaani na hivyo mtafiti amebaini kuwa ukosefu wa malezi mema ya watoto, husababishia watoto hao kuishia mitaani.

#### 4.4.4.3 Takriri

Takriri ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yaleyale kwa lengo la kutia mkazo au kusisitiza jambo. (Jilala, 2016). Kahigi na Mulokozi (1979), wakinukuliwa na Jilala (2016) anaesma, Takriri ni kuwa na uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata sentensi katika kazi za kifasihi.

Matumizi ya takriri katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* yamechangia kuweka msisitizo katika kukazia dhamira ya malezi kama ifuatavyo:

Aliinama tena na kumshika kwapa zake mbili. Alimburuta .**"Twende ! Twende! "**

**"Niache! Niache!"**

**"Twende ! Twende !"**

**"Niache ! Una laana mwanamke we!"**

**"Una laana mwenyewe!"…(**Uk.12)

Mwandishi wa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* ametumia mbinu ya takriri katika kusisitiza tabia chafu ya ulevi kwa baadhi ya wazazi hali inayoathiri malezi ya watoto ndani ya jamii. Mtafiti kupitia ukusanyaji wa data zake, amebaini kuwa

mama katika familia hujikuta anakosa mashirikiano ya kimalezi kwa mumewe na hatimae huathirika na kuchanganyikiwa katika maisha.

Tukirejelea nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa ishara unaohusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihi, ambapo msomaji wa kazi hii kupitia takriri zilizojitokeza, anapata ishara na kujenga kumbukumbu ya maisha ya wazazi jinsi yalivyo. Mbogo anaendelea katika matumizi ya lugha ya takriri kusisitiza dhamira kwa kusema:

Peter alimvuta, wakavutana. Na mara zogo likaanza tena. Mvutano uligeuka ugomvi, Peter na Kurwa: **Kukurukakara, Kukurukakara, Kukurukakara**. Watu**: hee! Hee! Leo! Leo! leo!Leo! Mambo leooo!** (Uk.61).

Mwandishi ametumia mbinu hii kuonyesha msisitizo wa ugomvi kati ya ndugu hao wawili. Neno '**Hee'** na '**Leo'** yamerudiwa mara kadhaa kutuchorea picha ya baadhi ya majirani kukosa imani, huruma na mapenzi kwa watoto na badala yake kushangilia ugomvi huo bila kujali hasara itokeayo. Hivyo takriri ni muhimu katika kujenga dhamira kulingana na mazingira aidha kusisitiza utendaji wa tendo jema au kinyume chake.

Mtafiti amebaini kuwa kulingana na wakati uliopo baadhi ya majirani/jamii hukosa mapenzi, huruma katika kuwalea watoto na kukinzana na msemo usemao kuwa "mwana wa mwenzio ni wako" Mtafiti anashauri kwamba, wazee, majirani na walezi kupendana na kushirikiana katika malezi ya watoto. Nadharia ya Sosholojia kupitia

msimbo ishara kumesaidia kumjengea picha msomaji wa kazi hii ili kuipata vyema dhamira ya malezi na kupata msisitizo katika kutambua aina ya malezi gani mema kwa watoto.

#### 4.4.4.4 Nahau

Mbogo ni msanii mahiri wa matumizi ya lugha ikiwemo nahau. Msanii huyu anaendelea kuipamba kazi yake katika matumizi ya nahau ndani ya riwaya yake ya *Watoto wa MamaN'tilie,* kwa kuingiza vionjo kutokana na nahau zilizosheni katika kazi yake. Senkoro (1982) anasema, Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambao huwa umesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno hayo katika matumizi ya kawaida. Nahau hutumiwa kupamba kazi za fasihi na pia katika kuwasilisha wahusika na lugha zao. Mbogo katika riwaya yake ametumia nahau mbalimbali kuwasilisha kazi yake kama anavyosema:

Wakati mzee Simango **akiupiga usingizi**, watoto watatu walikuwa macho. Hatua kama 40 hivi, nyuma ya mashine ya stima alichuchumaa Kurwa. Pale alipokuwepo aliweza kumuona mlinzi kalala. (Uk.43).

Mwandishi ameweka wazi jinsi watoto watatu (Doto, Kurwa na Dan) waliokosa malezi mema kujiingiza katika tabia ya wizi. Hivyo jamii inawajibu wa kufahamu kuwa katika malezi vikwazo viwapatavyo watoto ni vyema jamii ikajitahidi kuwasaidia watoto hao ili wasijiingize katika tabia ya wizi au tabia hizo mbaya. Aidha, mtafiti amebaini kuwa kila binadamu kwa nafasi yake anapaswa kushiriki katika malezi ya watoto, kuwaepusha kuingia katika tabia mbaya na kuwaelekeza

kupata elimu. Mwandishi ametumia nahau hii ya "kuupiga usingizi" kuonyesha jinsi mlinzi alivyokuwa amelala.

#### 4.4.4.5 Methali

Senkoro, (1982 na 2011) akinukuliwa na Jilala (2016) anasema: Methali ni semi fupifupi zinazobeba uzoefu wa jamii kuhusu maisha na hivyo kuadilisha na kuhekimisha jamii. Methali hutajirisha fani na maudhui ya kazi ya fasihi na hutumika kama daraja la kupitishia maadili kwa jamii husika.

Methali zina umuhimu mkubwa kisanaa katika kutajirisha maudhui na fani ya kazi ya fasihi. Katika riwaya hii ya *Watoto wa Mama N'tilie* methali zimetumika kujenga uhalisia wa mandhari inayoakisi dhamira ya umasikini katika familia husika. Kutokana na maelezo hayo methali imefafanua maudhui kupitia maana ya ujumbe uliobebwa. Katika riwaya hii anaonekana Maman'tilie kuchukua fedha za akiba kwa masikitiko, huku mwandishi akisema:

Alichukuwa kipochi kake kalikochakaa, akazitoa pesa zote. Alikuwa ameweka akiba kidogo kwa ajili ya watoto wake. "Sasa hili nalo! Ama kweli **kamba hukatika pembamba"** Maman'tilie aliwaza kwa masikitiko. (Uk. 34).

Mwandishi ametumia mbinu ya methali kutuonyesha dhamira ya malezi ya watoto jinsi yanavyokabiliwa na vikwazo kwa wazazi. Neno kamba linamaanisha jambo/tendo alilonalo mtu alilokusudia kulifanya, bahati mbaya Maman'tilie hakufikia malengo yake kwasababu, waswahili husema: Hamadi kibindoni silaha

mkononi. Maman'tilie ilimbidi kuitumia akiba yake ndogo kwenda kumualisa mama yake mzazi. Mbogo anaendelea kutumia mehali kuwasilisha dhamira ya malezi aliposema:

Hatimaye alisema, "Nimepata habari zako toka kwa Peter. Unasikia mtoto?" "Nasikia, dada" "Nimemkubalia Peter ukae. Hivyo, kaa! Lakini chunga! Isije kuwa **fadhila za punda.** Kaa hapa kwa heshima, wala usiwaletee sokomoko na patashika hawa wenzako. Unaelewa mtoto? "Naelewa, dada." (Uk.69).

Mwandishi ametumia methali hii, kumuasa mtoto Kurwa kuishi pamoja na wenziwe bila ya matatizo, isije kuwa fadhila ya punda mashuzi. Mtafiti amebaini busara, huruma na malezi mema waliyokuwa nayo wanawake kwa watoto. Kupitia nadharia ya Sosholojia katika msimbo wa kiishara, ni kwamba tabia za punda zinaashiria watu wenye matata/ wagomvi na ambao hawakubaliki katika jamii kupitia matendo yao. Sambamba na hilo jamii inahitajika kuachana na tabia za kipunda.

#### 4.4.4.6 . Misemo

Watunzi wa kazi ya fasihi, aghlabu hutumia misemo ya aina mbalimbali ambayo kwa dhamira mbalimbali huweza kufikisha kwa hadhira iliyokusudiwa. Senkoro (1982) anasema kwamba, misemo wakati mwingine hutambulisha mazingira maalumu au kuijulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa. Pia anaendelea kusema kuwa, misemo huzuka ama kuibuka na kutoweka kufuatana na hali mbalimbali za kimazingira.

Kwa hiyo matumizi ya misemo katika kazi ya fasihi hutegemea wakati mazingira maalumu na kuleta maana maalumu. Katika riwaya hii mwandishi ametumia mbinu hii maalumu ya kisanaa kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Mwandishi anasema:

Mjomba alisimama.“Haya,”aliwapa wapwa zake mkono wa heri. “Tutaonana.”

Hakuna aliyeulizia lolote kuhusu mzee Lomolomo. Mjomba alimjua shemeji yake kuwa ni **mtu wa maji,** si mtu wa kuwajibika. (Uk. 35).

Mwandishi ametuonyesha mazingira ya mhusika wake (mzee Lomolomo) kitabia ambayo ni maarufu kwa ndugu zake kiasi ambacho hana nafasi katika familia na jamii kutokana na tabia yake ya kilevi. Hapa mwandishi ametumia msemo huu katika kuipamba riwaya yake kwa kuwavutia wasomaji wake. Msemo uliotumika hapa ni kwamba mzee Lomolomo ni mlevi “Mtu wa maji.” Halkadhalika, mtafiti kupitia dondoo hii amebaini kuwa mtu mwenye tabia mbaya, hudharaulika ndani ya jamii yake na kukosa mapenzi. Kwa kuendelea zaidi, mwandishi ametumia misemo kwa lengo la kushadidia kuwasilisha dhamira ya malezi pale aliposema:

Maman’tilie alitoa vyombo, akapanda kitandani. Huyu ndie mzee Lomolomo, Lomolomo mpya ambaye kwake **pombe ya mataputapu na gongo alivifanya dini,** tangu alipopunguzwa kazi kule Bandarini na kukosa kabisa kibarua kingine. (Uk.13)

Dini ni imani ya mtu kumuabudu Mungu wake. Mwandishi amemshabihisha mhusika mzee Lomolomo na tabia yake ya ulevi wa kupindukia kuwa ni ibada kwake. Sababu iliochangia mhusika huyu kujenga hulka hii ni kule kupunguzwa kwake kazini na kukosa mwelekeo wa kimaisha. Mwandishi ametuonyesha dhamira

ya malezi ya watoto kwa mzazi kukosa kutumia mbinu mbadala kujikwamua kimaisha katika familia baada ya kukosa au kuondoshwa katika kazi ya mwanzo. Mtafiti amebaini kuwa ni budi jamii kubadilika kiuchumi ili iweze kujikimu kimaisha na kuwajengea watoto wetu misingi bora kimalezi kwa lengo la kuwapatia haki zao zote.

### 4.4.4.7 lugha ya Kitaharuki

Wasanii wa kazi za fasihi wanapenda kutumia mbinu ya taharuki ili kuwavutia wasomaji waendelee kuzisoma kazi zao.Wamitila (2002) anasema kuwa, taharuki inaleta hamu ya kujua na kutia hamasa ya kupenda kusoma zaidi.

Senkoro (2006) anasema: Taharuki ni ile hali ya kuchelewesha matukio fulani au majibu ya maswali fulani ambayo msimuliaji hufanya yawazukie wasikilizaji au watazamaji wake. Haya hucheleweshwa hadi baadaye sana wakati ambapo hadhira huwa imekwishanig'inia katika kamba ya taharuki kwa muda mrefu.

Wasanii waliobobea katika kazi za fasihi mara nyingi hupendelea kuichora taharuki mwishoni mwa kazi zao ili kumfanya msomaji aweze kutafakari alichokisoma na kuweza kufikisha dhamira ya mwandishi. Haya yamejitokeza katika riwaya ya *Watoto wa MamaN'tilie* kama ifuatavyo:

Maman'tilie, Mama Sara na Zenabu, wakiwa wamejawa na machungu ya Zita moyoni mwao, nao walishuka. Mmamn'tilie, ambaye tangu Muhimbili alikuwa kimya, sasa aliinua mikono na kujitwika kichwani. Alipasua kilio huku akikimbia,

"Zita ! Zita! Zita Oh! Zita umekwenda! Umenitoroka, Zita mwanagu, Oh! Mungu wee! "Mbio! Alikimbia Mamantilie. Mbio! Mbio! Akakata vichochoro vya Manzese ! Zenabu na Mama Sara nao walikuwa hatua moja nyuma yake. Watu mitaani waliacha waliyofanya, wakawa wanamtazama mama yule aliyekuwa akilia kwa yowe. Walipokaribia nyumbani hata Mama Sara na Zenabu hawakuweza kuvumilia zaidi. Nao walitokwa na milazamu ya machozi, wakilia na kugutia, Zitaeee! Zitaeee! Mamantilie mbele, wao nyuma. Loo! Umati! Kaya ya mzee Lomolomo ilijaa waombolezaji. Waliokuwa wanalia au kuongea pale nje ghafla walinyamaza. Wimbi lile la watu liligeuka kuwatazama wanawake watatu waliokuja mbio, mikono vichwani, nguo zikiwavuka, wakilia na kugutia, Zita weee! Kurwa ndiye aliyekuwa wa kwanza kuwalaki. Alikimbia mbele, kelele za yowe mdomoni, "Baabaeee! Baba amekufaaa!"

Mama Sara alipasua kilio,"Zita, mwanangu umetutokaaa!" Hakumwelewa Kurwa. Wimbi hilo la watu likapatwa na wazimu. Wanaume walipata taabu kuwatuliza watu. Maman'tilie alikimbia akilia. Alifululiza hadi chumbani. Wanawake kadhaa walimfuata nyuma. Chumba bado kilikuwa kinafukuta harufu mbaya.…aliutazama lakini mwili ule uliona aibu, ukawa umefumba macho. Maman'tilie alimkumbatia mumewe, "Baba! Baba watoto? Mwenzangu! Ee! Amka! Simama! Usiniache! Usiniachie tanzia hii peke yangu! Nakwambia Zita hayupo tena " (Uk.92-93).

Mwandishi ameiweka taharuki katika sura ya mwisho kwa namna ya kumvutia msomaji kupata mori na hamu ya kuisoma kazi yote ili kujua ni kitu gani kitakachotokea kwa wahusika wa riwaya hii na kuibua maswali mengi yanayohusu

dhamira ya malezi na hatimae kuelewa kwamba, umasikini katika familia kumeibua madhila, vifo na taharuki kwa familia iliyochafuliwa kutokana na ukosefu wa malezi mema kwa watoto na uzembe wa wazazi mfano Mzee Lomolomo, kumewaumiza watoto wake nakuwasababishia vifo visivyotarajiwa na kifungo jela (Peter), hatimae kumuweka Mamantilie kurudi nyuma katika harakati zake za kujikwamua kimaisha na kuachiwa majonzi na upweke!

Kwa kuendelea zaidi, Mbogo ameendelea kutudhihirishia taharuki katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* kupitia wahusika wake Kurwa, Peter na Mussa. Mwandishi anaposema:

> "Keleleee! Ndugu, ndugu! Mii ndugu yako!". Aliwatia pingu. Sasa watoto wote wakaanza kulia kwa sauti. Na huko nje watu wakaanza kujazana Waswahili hawana dogo. Kurwa alisema, "Bwana polisi nisikilize tafadhali" "Wachaa!" alisema akiwasukuma hadi nje.
>
> "Sikiliza! Sikiliza nakwambia !" Kurwa alipandisha hasira na kusema kwa nguvu bila kujali. Na kweli polisi walionekana kustuka. "Nini we mtoto! Twende! Utasema yote hukohuko korokoroni!" "Nasema sikiliza ! Baba amekufa ! Zita amekufa! Mimi nimetumwa nije kumwita huyu kaka yangu. "… Lakini Kurwa alilia, "Haki! Jamani tuachilieni"… (Uk.98)

Kwa kawaida mbinu ya taharuki inamfanya msomaji kuingiwa na shauku na kujenga udadisi juu ya kitakachoendelea katika hadithi ili kupata dhamira ndani ya riwaya teule.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kihemenetiki unaohusu taharuki na usimulizi, kumemuweka msomaji kutambua nafasi ya watoto kutosikilizwa na askari baada ya kukamatwa.

Mtafiti amebaini kuwa, haki ya watoto ya kusikilizwa imetenguliwa hali inayowasononesha na kuwazidishia machungu watoto hao, pamoja na hayo mtafiti kupitia vyombo vya dola anaipongeza serikali kwa kuwajibika kuwakamata watoto wanaojishuhulisha na matumizi ya madawa ya kulevya, kwani serikali ndio mlezi mkuu wa watoto nchini kwa kuwaundia na kuzisimamia sheria zinazowalinda watoto hao na kuwawajibisha pale inapothibiti kuwa wanametenda kosa.

Kwa msingi wa kurejelea swali la msingi la kwanza linalokwenda sambamba na lengo mahsusi la kwanza, mtafiti amebaini kuwa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* imesheheni mbinu lukuki za kisanaa ambazo zilitumika kujenga dhamira ya malezi katika riwaya teule. Hivyo basi ni imani ya mtafiti kuwa riwaya hii bado ni lulu katika ujenzi wa mbinu hizo za kisanaa ambazo zinafanikisha vyema kazi hii ya mtafiti inayohusu dhamira ya malezi ya watoto.

## 4.5 Dhamira ya Malezi Katika Riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie

Ni dhana isiyo na shaka kuwa sifa ya mwandishi hutoka ndani ya jamii anayoiandikia, hivyo, Emmanuel Mbogo kwa kurejelea riwaya yake ya *Watoto wa Mama N'tilie*, amekereketwa na tabia ya baadhi ya wazazi, walezi na jamii yenye kukinzana na sheria inayomlenga na kumlinda mtoto dhidi ya changamoto mbalimbali anazokutana nazo ikiwemo kukosa haki zao za msingi kama: chakula, mavazi, elimu, malazi, matibabu, pamoja na haki ya kuburudika na kucheza n.k. Riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* imekwenda sambamba kufanikisha kazi ya mtafiti kwa kiwango kikubwa kwa kuichunguza dhamira ya malezi ya watoto kupitia riwaya teule. Mtafiti amesoma na amezingatia kwa kina lengo mahsusi la pili la

utafiti huu lisemalo: (ii) Kuchambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Lengo mahsusi hili la pili limekwenda sambamba na swali la msingi la pili la utafiti huu lisemalo: Ni dhamira zipi za malezi ya watoto zilizojitokeza katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tiliye?*

Kwa kuzingatia lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiiti huu, mtafiti amebaini dhamira hizo za malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* akihusisha na nadharia ya Sosholojia kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Malezi ya Watoto kwa Baba na Mama (Malezi ya Familia)

Wazazi huwa wanafunganishwa na ndoa ambapo huwa tayari wamekubaliana kisheria kwa mujibu wa taratibu za mila na desturi za kikabila au dini husika, kuishi pamoja kwa raha na shida. Katika jamii nyingi za Kiafrika pamoja na ulimwenguni kote suala la ndoa linaheshimiwa na kupewa baraka na wazee kwa kujua kwamba ni matokeo ya mapenzi ya bibi na bwana.

Matokeo na baraka ya mapenzi haya ndani ya ndoa, ni kujaaliwa na Mwenyezi Mungu baraka ya kizazi ambapo watoto huzaliwa ikiwa ni hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, ni wajibu wa wazazi husika kuwalea vyema kwa mapenzi, na kuwapatia mahitajio yao muhimu yakiwemo: Lishe bora, elimu bora, afya, mavazi, malazi, kuwapa maadili mazuri n.k. kwa ajili ya kuwakuza kimwili, kiakili na kiroho kwa lengo la kuwa na familia, jamii na taifa bora la baadae.

**Malezi Mema:** Katika utafiti huu mtafiti amebaini kuwa maisha ya wahusika katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* iliyoongozwa na Mzee Lomolomo na mkewe Maman'tilie, pamoja na watoto wao, Peter na Zita. Watoto hawa walipata malezi mema, yenye kujua thamani ya wazazi hasa mama kwa kupata upendo, huruma, furaha na amani. Mtafiti ameligundua hili kama mwandishi anavyosema:

> Mama aliita, "Zita wee!" "Bee, mama." "Ebu washa jiko tupike."
>
> "Ndiyo mama" Zita alichukua jiko, akajaza mkaa; kisha akachukua mafuta ya taa kwenye chupa …
> "Wewe! Haya ! Rudisha hayo mafuta, alaa ! Unataka tulale giza sie? "
> "Jamani, Mama!" Zita alinung'unika.
>
> "Jamani mama nini? Washia karatasi. Kachukue kiberiti chumbani"
>
> Saa mbili usiku ugali na maharage ulikuwa tayari. Maman'tilie na wanawe wawili walikaa, wakala, wakanywa maji, wakamshukuru Mungu. (Uk.7).

Mtafiti amebainisha kuwa, malezi mema ya watoto hutegemea uwepo wa wazazi wenyewe, husaidia kuwafunza watoto wao tabia nzuri na kuwapa mafunzo mema, kama Maman'tilie alivyokuwa anamfunza mtoto wake. kuwa na matumizi mazuri ya mahitajio yao ya nyumbani, Sambamba na kuwalea watoto hao kuwa karibu na wazazi wao.Kwa kurejelea nadharia ya Sosholojia, kupitia muhimili wake, mzazi kuwa ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, (uhusiano wa mzazi na mtoto): Mtafiti amebaini dhana nzima ya mzazi (mama) kufanya juhudi za kumshirikisha mtoto wake katika kutambua maisha halisi kwa mujibu wa mazingira wanayoishi. Sambamba na hilo watoto hujihisi furaha, amani na upendo kwa kukaa pamoja na wazazi wao. Mashirikiano makubwa ya mama na mtoto wake Zita tangu kutayarisha chakula hadi tendo la kula pamoja, tendo ambalo husaidia wazazi kuwafunza watoto

heshima na adabu za kula kwani hata dini zote zinahimiza hivyo. Pia mwandishi ametuonyesha malezi mazuri baina ya baba na mama. Mwandishi anasema:

> Mama alihimiza, “Haya! Tembeeni upesi. Tunachelewa hivyoo! ”
> Yule msichana akasema, “Mama, baba ataninunulia gauni la krismasi? ”
>
> Mvulana akadakia, “Mama, mimi nataka raba za kuchezea mpira.” (Uk.37-38).

Mwandishi ametudhihirishia kuwa suala la malezi ya watoto ni la wazazi wawili, kwani watoto hao walionyesha furaha, upendo na kuwa huru huku wakidai mahitaji yao kwa wazazi wao. Kulingana na nadharia ya Sosholojia katika muhimili wake unaomuhusisha mzazi kuwa ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora: Mwandishi amezungumzia juu ya yale ambayo yanaakisi ukweli katika jamii tunayoyaona yanatendeka kila siku kwa kuwa fasihi huwakilisha maisha kwa upana wake hususan uhalisia wa kijamii, hivyo mwandishi amewakilisha wazazi wenye malezi bora kwa watoto.

**Ukosefu wa Mashirikiano katika Malezi:** Suala la kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri kati ya baba na mama, nalo pia mtafiti amelibaini kuwa limechangia watoto kukosa malezi bora, Mzee Lomolomo (baba), ni mlevi wa kupindukia na ndie chanzo cha kutokuwepo kwa mashirikiano, jambo ambalo lilimpelekea Maman’tilie kushindwa kuyamudu maisha inavyostahiki kwa kukosa kuwapatia watoto wake mahitajio ya shule ikiwemo ada na sare za shule, lishe bora, huduma za afya n.k, suala ambalo liliwapelekea watoto hao kukosa haki zao za msingi, ikiwemo haki ya kupata elimu. Mwandishi anatueleza;

> “ Zita alisema, Mwalimu Mkuu kasema wote ambao hawana nguo za shule wala hawajalipa ada asiwaone shule tena .”
> Peter akaongeza, “Kwa hiyo mama ufanye bidii ututafutie pesa ili tununue sare na turudi shule”
>
> “Mambo hayo muwe mnamwambia baba yenu. Si mimi” (Uk.6-7)

Mtafiti amebaini kwamba baba ni nguzo ya familia, pale ambapo Maman’tilie aliwajibu watoto wake kuwa taarifa za kufukuzwa shule wamuarifu baba yao na sio yeye. Lakini watoto hao hawakokaribu na baba yao mzazi kiasi ambacho mahitaji yao yote humuelekezea mama yao mzazi, kutokana na kutowajibika kwa baba mzazi katika familia hii, tabia yake chafu ya ulevi wa kupindukia kumesababisha kuwakosesha watoto Zita na Peter haki yao ya kupata elimu, kulikowapelekea kuishia katika mikono mibaya, mfano, mtoto Peter kukamatwa na askari polisi kwa kosa la kuuza madawa ya kulevya na kusekwa gerezani.

Pia ukosefu wa mashirikiano katika malezi ya watoto humuathiri sana mama kwasababu ndie mlezi nambari moja. Mwandishi anasema:

> “Baridi ya huzuni ilimwingia moyoni, alifikiri juu ya elimu ya watoto wake. Pesa alizokuwa anazipata kwa kuuza ugali na maharage kule Kiwanda cha Urafiki hazikutosheleza matumizi ya nyumbani, sembuse ada na sare za watoto! Mumewe mzee Lomolomo alikuwa lofa mtu wa kazi za kijungujiko na vipesa vyake vilivyoishia kwenye pombe za chang’aa au gongo ” (uk 6-7.)

Vilevile, mtafiti amebaini kuwa, changamoto ya kukosa kuwajibika na ukosefu wa mashirikiano baina ya wazazi unachangia kuwakosesha watoto malezi mema jambo ambalo ni hatarishi kwao katika familia, jamii na taifa kiujumla.

Katika jitihada za mama Zita kujikwamua kiuchumi, kwa lengo la kuiokoa familia yake na huduma mbalimbali kama shule n.k. Mtafiti amebaini kuwa mwanamke ni kiungo muhimu katika familia, ni mpiganaji mahiri katika malezi ya watoto, ingawa anakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha. Mtafiti amegundua kuwa, suala la malezi limezua mjadala mkubwa sana katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie,* ni kweli baadhi ya wazazi katika jamii wamejisahau katika jukumu la kuwalea na kuwaongoza watoto. Jambo hili, kwa kiasi kikubwa limechangia sana katika kuporomoka kwa malezi na kuzorota kwa maadili ya watoto jambo linalowapelekea kujiingiza katika: ulevi, utumiaji wa madawa ya kulevya, wizi, ujambazi.n.k.

Kwa upande wa nadharia ya Sosholojia kupitia mhimili wake unaokuza mahusiano mema baina ya mtu, watu, jamii na taifa: inaitaka jamii kuwa na mashirikiano miongoni mwao katika kukuza malezi, maadili na matunzo mazuri ya familia.

### 4.6.1 Malezi ya Watoto kwa Majirani

Jirani ni ndugu ambao wanaishi kwa pamoja kwa kushirikiana kwa hali na mali wakiwa wanapendana, kuoneana huruma,n.k. Katika utamaduni wa kiafrika, ni jambo la kawaida kwa jamii zetu kuishi kwa kusaidiana katika nyanja mbalimbali zikiwemo: malezi, kilimo, uvuvi, misiba, harusi n.k.

Suala la malezi ni jukumu kwa wazazi/walezi pamoja na watu mbalimbali katika jamii husika. Mtoto anapozaliwa, hulelewa na familia akiwemo baba na mama,walezi huongezeka kwa kuwa mtoto atakuwa ameingia kwenye hatua

nyengine ya makuzi na kulelewa katika jamii inayomzunguka, mfano majirani, walimu na ndugu wengineo.

**Majirani Wema:** Katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*, mwandishi hakuwa nyuma kuwakilisha nafasi ya jirani katika malezi ya watoto kwa nia ya kuwajengea misingi iliyotukuka. Mwandishi kwa kulidhihirisha hili amewatumia wahusika wake Zenabu, Mama Sara na Jane wakiwa ni majirani wema kwa familia ya Maman'tilie. Mbogo anasema hili kama ifuatavyo:

> " Mama Zita, ee! " sauti ya jirani yake, Zenabu kasimama nje ya nyumba.. Alipaza sauti, "Vipi homa yako, mama?" (uk.5)

Katika ukusanyaji wake wa data kupitia riwaya hii mtafiti amebaini kuwa, kuishi vizuri na majirani hujenga mapenzi, udugu na kusaidiana kwa wema. Hivyo ni vyema kwa majirani kuulizana hali kabla ya kila mmoja kuanza harakati zake za kimaisha.

Mwandishi anaendelea kuelezea umuhimu wa malezi ya watoto kwa majirani kama:

> "………..Mara sauti ilimwita, "Peter wee!" Peter aliitikia. Alimwona Zenabu kasimama nje ya chumba chake. Aliinuka, akaenda "Shikamoo dada"…"Marahaba.Vipi?"…"A-aa!" alitingisha kichwa. Zenabu aliona ile midomo mikavu iliyokaukiana. Aliuona uso ule ulioparama na macho yenye tongotongo bado. Aliona miguu ile pekupeku yenye ngozi iliyokatika ikiwa migumu kama ya mamba. Zenabu alisema, "Hata kunawa hujanawa." Peter alitazama chini, dole lake gumba linachora mistari aridhini. Zenabu aligeuka,"Njoo unawe."Alimpeleka Peter uani, akampa maji. Peter alinawa uso akarudi chumbani. "Kaa". Peter alikaa kwenye kiti maji bado yanamvuja usoni. Zenabu alimmiminia chai ya rangi kwenye kikombe cha plastiki. "Haya, kunywa! "Peter hakuichukua chai ile mara. Badala yake aliikausha mikono yake kwenye kaptura. Macho

> yake yalimwangalia Zenabu akipakua sahani ya muhogo. Alimwekea mezani. “Kula uende kucheza.” “Asante”… (Uk.14 -15.)

Ni sifa ya binadamu kuwa na tabia njema miongoni mwetu, mtafiti amebaini hayo kupitia taasisi za kidini kuhimiza waumini kuwa na upendo kwa watoto.Mtafiti amelithibitisha hilo kupitia mwandishi pale alipomsawiri Zenabu kuwa na sifa njema, mapenzi, huruma kwa watoto kwani wahenga wamesema “Mzazi ni mmoja lakini walezi ni wengi.” Watoto hujenga upendo, imani, na ukaribu kwa wazee/majirani wenye kuonyesha mapenzi na kuwajali hasa wanapokuwa na dhiki. Kwa kurejelea nadharia ya Sosholojia kupitia muhimili wake unaokuza mahusiano mema baina ya mtu, watu, jamii na taifa: Mtafiti anaona ni vyema kuishirikisha jamii katika kuwapa malezi mema watoto, watakaojenga taifa lenye upendo na misingi imara kwa maendeleo ya nchi.

Mbali na hayo mwandishi anaendelea kufafanua juhudi za majirani wema, kwa kumrejelea mhusika Zenabu katika malezi ya watoto wa jirani kwa kusema:

> …… “Sema upesi Peter. Una mpango gani? ”Peter aliona heri aeleze. “Dada, kweli mchele huu nimetoka nao dampo. Nataka nipate pesa, nirudi shule.” Alinyamaza kidogo akisubiri Zenabu aseme kitu lakini alikaa kimya. “Nataka uufiche. Usimweleze mama mpaka nitakapokuwa tayari”
>
> Zenabu aliyajua maisha ya watoto wengi wa aina hii hapa jijini. Wengi waliishia katika uchokoraa, wizi, ujambazi, kula mirungi na kuvuta bangi. “Hapana,” Zenabu aliwaza. “Huyu mtoto alikuwa ameteleza, lakini hajaanguka.”… “una njaa” “Sana dada.”
>
> Zenabu alisimama akampa ugali na samaki aliobakiza.“Nenda uwani unawe, ule” … “Haya Peter siri yako nitakufichia. Ila sitaki vitu vya wizi hapa nyumbani kwangu. Unaelewa?” Peter alitikisa kichwa ishara ya kukubali….“Naelewa dada” Alimaliza kula akasimama ili atoe vyombo. “Viache vyombo vyangu. Kimbia nyumbani kwenu

> ukaoge. Tazama! Unanuka! "…Peter alishukuru, akatoka kurudi kwao. (Uk. 31).

Mapenzi na malezi mema kwa watoto yanayofanywa na baadhi ya majirani katika jamii zetu husaidia kumjenga mtoto kiimani na kumpa upendo. hii ni sawasawa na msemo usemao kuwa "Mtoto wa mwenzio na wewe ni wako". Kutoa neno la shukran "Asante " ni sehemu ya utamaduni baada ya kupewa kitu chema na mwenzio/mzazi, kama alivyofanya Peter baada ya kukirimiwa chakula na Zenabu.

**Mashirikiano kwa Majirani:** Kwa kuendelea na dhana ya malezi ya watoto, jirani ni sehemu ya familia na kufanya mfumo ndugu wa malezi, kama mwandishi alivyotuonyesha kupitia mhusika Zenabu jinsi anavyoshirikiana vizuri na Maman'tilie katika kumsaidia malezi mema kwa Zita na Peter, mwandishi anasema:

> Zenabu alikuwa keshaupodoa, tayari kwenda kazini. Pale mlangoni alimwona Maman'tilie."Mama Zita shikamoo."…"Marahaba""Wapi safari?...Oh! Mjomba?"…Walisalimiana na mjomba. Maman'tilie alimchukua chemba, akanong'ona,…"Zenabu mie naenda nyumbani. Mama yu mahututi. Tafadhali nitazamietazamie wanangu mara mojamoja. Zenabu alijibu,"Nitawaangalia mama. Mgonjwa nini cha mno?... (U.k.35)

Nadharia ya Sosholojia kupitia msingi wake wa umahususi na sio umajumui, inaitaka jamii kujikita kwenye utamaduni wa jadi, yaani kusaidiana na kushirikiana katika malezi ya watoto na nyaja muhimu zote ikiwemo harusi, ugonjwa na hata misiba nk. Msanii anaendelea kudhihirisha umuhimu wa mashirikiano katika malezi kwa majirani baada ya Zita kuugua homa ya kichaa cha mbwa na majirani kumsaidia. Mwandishi anasema:

> Zenabu alisimama, "Jamani nisaidieni! Mnacheka nini wendawazimu wakubwa! Hamwoni kuwa huyu mtoto ni mgonjwa!" Baadhi ya

> watazamaji wakamzomea, “Aaa! Nini we mwanamke! Mwendawazimu mwenyewe!”…Lakini mara Mama Sara alifika. Zenabu alipomwona, alisema, “Mama Sara nisaidie mwenzangu” “Loo! Imekuwaje!” “Malaria! Imempanda kichwani. Mshike nikimbie nilete teksi”…Mama Sara alimshika Zita kiunoni. Zenabu aliingia chumbani kwake, akachukua akiba yake ya pesa. Huyoo!...(Uk.82-83)

Majirani wamechukua nafasi ya mzazi bila ya kujali kwa kumuhudumia Zita na kumkimbiza hospitali. Mtafiti anashauri kuwa tabia hii ni vyema kuendelezwa katika jamii, kwasababu jambo hili huzidisha mapenzi baina ya majirani, wahenga walisema: Akufaae kwa dhiki ndie wako rafiki. Hivyo kwa kurejelea nadharia ya Sosholojia katika mhimili wake wa dhima kwa kijamii unaoakisi uhusiano baina ya watu: Dhima hii pia itazidisha mapenzi na mshikamano katika malezi ya watoto na kuzuia madhara mbalimbali ambayo yanayoweza kuwakumba watoto ikiwemo magonjwa, matumizi ya madawa ya kulevya, utoro mashuleni, wizi, mimba za utotoni n.k.

Mbogo anaendelea kutuonyesha mfumo ndugu wa majirani kwa kutuchorea namna gani wanavyosaidiana katika malezi ya watoto pale mama mzazi anapoaga dunia na kuacha watoto mayatima mfano, Mama Kurwa baada ya kufariki watoto wake (Kurwa na Doto) walilelewa na jirani yake ambae ni Jane. Mbogo anaeleza:

> Siku ilipofika saa 8:02 usiku, Mama Kurwa alikata roho. Japo Jane, hakujaaliwa mtoto, sasa alikuwa na watoto! Ilibidi awalee watoto wa marehemu rafiki yake. Na polepole jina la Jane likafa. Wakazi wa Kisutu wakawa wanamwita Mama Kurwa. Ilikuwa kama kafa, kisha Mama Kurwa kafufuka tena! (Uk.37)

Mtafiti amebaini kuwa mtoto halelewi na baba na mama tu, bali asasi nyenginezo hushiriki katika malezi ya watoto wakiwemo majirani. Ni ukweli usiopingika kuwa

utamaduni wa Mwafrika kabla ya majilio ya wageni na elimu ya Kimagharibi, malezi ya watoto pia yalikuwa ni malezi kwa wanafamilia, majirani na jamii kwa ujumla. Tabia potofu miongoni mwa watoto zilishutumiwa na kupigwa vita na jamii nzima, hivyo mtoto anapokosea huhukumiwa hata na jirani tu. Ingawa matendo haya kulingana na mabadiliko ya wakati, jamii na mazingira halisi suala la malezi ya watoto limekumbwa na wimbi la taharuki za maisha na wazazi/walezi na hata majirani kujikuta kuwa mbali na watoto wao/familia zao.

**Malezi mabaya:** Si jambo geni kwa baadhi ya watu kupenda kumuona mwenzake kafikwa na maovu,hali inayochangia malezi mabaya kwa watoto. Baadhi ya majirani kushangiria maovu yanayofanywa na watoto mitaani, mfano ugomvi, wizi n.k, badala ya kuwakemea. mwandishi anasema:

> Hakuamini macho yake. Pale kwao nje walijaa watu tele wakiangalia senema, kelele na zogo mtindo mmoja. Kulikuwa na nini? Peter alijiuliza. Alipopenya katikati ya kundi la watu. “Nipishe ! nipishe! Nipisheni, ala!” “Ala ! Mwenyewe watu walimjibu.
>
> Peter hakujali, alisonga mbele! Katikati ya dimba aliwaona Zita na Kurwa wanapigana miereka, nguo zao zimeraruka. Kurwa vidonda vyake vimefumka upya, vinatema damu. Zita nywele timtim, mdomoni tambuu na puani kamasi nyekundu. Kama kawaida ya watu wa mjini, hakuna aliyewaamua. Walihimiza, wakacheka na kutia maneno ya kishabiki “Waache! Waacheni tuone leo! Heeee !” (Uk. 60).

Ni dhahiri kuwa kazi ya fasihi huathiriwa na wakati pamoja na mazingira halisi ya kijamii, mtunzi ni mwanajamii kwa maana ana nafasi na tabaka fulani katika jamii yake (Ntarangwi 2004). mtafiti amebaini kuwa, tabia mbaya za baadhi ya majirani huchangia na kuharibu malezi ya watoto. Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia,

kupitia msingi wake wa umahususi na sio umajumui, kazi ya fasihi ni kiwakilishi halisi cha jamii husika.

### 4.6.2 Malezi ya Watoto Shuleni

Shule ni miongoni mwa taasisi zinazojikita katika kutoa malezi na maadili mema kwa watoto, ambapo wazazi huwapeleka watoto wao ili wapate elimu, malezi na maadili mazuri kwa ujumla. Mlezi mkuu wa watoto shuleni ni mwalimu ambae huchukua nafasi ya mzazi wakati anapokuwa shuleni. Serikali ndio muhimili mkuu kwa kusimamia, kufuatilia na kutoa huduma muhimu mbalimbali kwa wananchi wake ikiwemo elimu, kwa maslahi ya watoto, jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie,* Mbogo hakusita kutuonyesha taasisi ya serikali ambayo ni shule, kuwa ni miongoni mwa taasisi ya malezi ya watoto ambayo walezi wake hutokana na jamii husika. Mtafiti kupitia uchambuzi wake wa data alizokusanya amebaini kuwa taasisi hii haikuwatendea haki watoto waliofukuzwa shule kwa sababu tu ya kukosa ada na sare za skuli. juhudi za serikali hii tukufu ni kuhakikisha kuwa haki na ustawi wa watoto unazingatiwa katika kila nyanja ya kijamii na kwamba masuala ya mtoto yanapewa kipaumbele. Mfano wa haya mwandishi anasema:

> Ilikuwa saa 10:30. Walimu wa Shule ya Mapepela walikuwa wamewaruhusu wanafunzi warudi nyumbani. Mwalimu Mkuu, Mwalimu Chikoya aliwatangazia wanafunzi, "Wote ambao hamjalipa ada na hamna sare, hakuna shule! Nisizione sura zenu bila ada na sare .Waambieni wazazi wenu hivyo " (U.k.1 )

Bila ya shaka, mtafiti amebaini kuwa uvunjwaji wa sheria na kutokuwa makini kwa baadhi ya viongozi kwenye taasisi zao husababisha haki za msingi za watu

kuvunjwa. Mfano, mwalimu Chikoya, Vilevile mtafiti amebaini kuwa umasikini kwa jamii isiwe chachu ya kuwakosesha watoto elimu, badala yake serikali ibebe jukumu hilo.

Hata hivyo, mtafiti amebaini kuwa kupitia serikali iliyopo madarakani, chini ya uongozi wa raisi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, imeondoa gharama za malipo kwa wanafunzi wote nchini jambo ambalo linasaidia kuondoa ugumu wa kupata elimu.Uhaba wa walimu na vitendea kazi, ni changamoto kwa serikali, vilevile walimu wasiwahukumu watoto kwa kukosa ada, bali warudi kwa waajiri wao kupeleka malalamiko hayo. Kwa kuzingatia nadharia ya Sosholojia katika msingi waelimu na maendeleo kwa jamii:Ni vyema serikali iwapatie watoto elimu bora pamoja na kusaidia familia za wanyonge (masikini) kufanikisha ndoto za watoto hao.

**Mapenzi ya Shule:** Elimu humsaidia mtoto kupata malezi mema kwa jamii, athari ya saikolojia hupelekea mtoto kujiingiza katika makundi maovu wakidhani kuwa ni njia pekee ya kujinsua kimaisha, mfano kujiingiza katika wizi, madawa ya kulevya, n.k. Mwandishi amelibaini hili kupitia muhusika Peter kama ifuatavyo:

> “Zita alisema, Mwalimu Mkuu kasema wote ambao hawana nguo za shule wala hawajalipa ada asiwaone shule tena” Peter akaongeza,“Kwa hiyo mama ufanye bidii ututafutie pesa ili tununue sare na turudi shule”(uk.6-7)

Ukosefu wa elimu kutokana na hali duni ya maisha iliyochangiwa na ulevi wa mumewe mzee Lomolomo kwa watoto wake kukosa elimu. Suala hili

lilimuhuzunisha mwilini mwake Maman'tilie kama alivyotudhihirishia mwandishi kwa kusema:

> "Baridi ya huzuni ilimwingia moyoni, alifikiri juu ya elimu ya watoto wake. Pesa alizokuwa anazipata kwa kuuza ugali na maharage kule Kiwanda cha Urafiki hazikutosheleza matumizi ya nyumbani, sembuse ada na sare za watoto! Mumewe mzee Lomolomo alikuwa lofa mtu wa kazi za kijungujiko na vipesa vyake vilivyoishia kwenye pombe za chang'aa au gongo " (Uk 7)

**Vikwazo vya Elimu:** Mtafiti amebaini kuwa kupitia Suala la ubadhirifu kwenye sekta za serikali, pia huchangia kuwakosesha watoto haki zao. Mfano wa haki ya msingi wanayoweza kuikosa watoto ni haki ya elimu. Kitendo cha baadhi ya wafanyakazi (Askari wa jiji) kupenda kula rushwa hasa kutoka kwa jamii yenye kipato cha chini ambayo hujitahidi kufanya kazi zao kihalali hukwamisha juhudi za maendeleo yao na watoto. Mwandishi amelidhihirisha hili kwa kusema:

> Takriban mwezi mmoja ulikuwa umepita. Pamoja na juhudi za biashara, Maman'tilie alikuwa bado hajafanikiwa kupata pesa za kutosha. Kodi na hongo kwa askari wa jiji zilikamua faida yake. Matibabu kwa homa na matumbo ya kuhara vilitafuna kiasi kilichobaki. Chakula cha nyumbani na kodi ya nyumba vilitishia kumeza hata mtaji wake mdogo. Fedha za shule zingetoka wapi? Hivyo, Peter na Zita waliendelea kukaa nyumbani. (Uk.32)

Ni ukweli usiopingika kuwa fasihi ni amali ya jamii, mwandishi huibua wazo litokanalo na jamii yenyewe na kulifikisha kwa hadhira /wasomaji. Kinachotakikana kwa msanii ni kuwa na jicho pevu la ndani ya jamii yake kufichua maovu yanayojitokeza kwa baadhi ya watu katika kukwamisha maendeleo ya jamii husika. Mtafiti amebaini kuwa, baadhi ya watumishi katika serikali hukosa maadili kiasi ambacho jamii ya watanzania imekithiri uozo wa rushwa, kiasi cha wasanii kushindwa kulifumbia jicho suala hili. Swali la rushwa kwa kweli ni maumivu na

mwiba mkali kwa taifa changa la kesho (watoto). Ni hatari iliyoje kwa watoto kukosa haki zao za kupata elimu kwa tamaa ya wachache wasio na huruma wala kujali maendeleo ya taifa na viongozi wa baadae. Hivyo mtafiti anashauri kuwa wafanyakazi wenye tabia hizi wawajibishwe bila la kuonewa haya.

Nadharia ya Sosholojia katika msingi/mhimili wake unaohusu elimu na maendeleo ya jamii, unaeleza kuwa suala la umuhimu wa shule (elimu kwa ujumla wake) lina thamani kubwa katika kujenga taifa bora na imara la baadae. Vilevile nadharia ya Sosholojia inafungamanisha fasihi na jamii (Njogu na Chimerah 1999), ni dhahiri kuwa malezi mema ya watoto yatajenga jamii na taifa bora ikiwa ni pamoja na kuzingatia elimu.

Kwa upande mwengine mwandishi amesawiri picha ya Peter kuwa na hamu ya kutaka kuendelea na masomo kwani alikuwa mbunifu katika kutafuta pesa za kujikimu shuleni, mwandishi anasema:

> Peter aliona heri aeleze. " Dada, kweli mchele huu nimetoka nao dampo. Nataka nipate pesa, nirudi shule" Alinyamaza kidogo akisubiri Zenabu aseme kitu lakini alikaa kimya. "Nataka uufiche, usimweleze mama mpaka nitakapokuwa tayari." (Uk.31)

Mtafiti amebaini kuwa watoto ni watundu katika kufanikisha wanayoyataka na huwa wabunifu katika kupata kile wanachokitaka, mfano elimu, n.k. Peter alikabiliwa na vikwazo mbalimbali kama, umasikini, ulevi kwa baba yake n.k, vilivyompelekea kushindwa kuipata haki yake ya elimu. Hivyo alijitahidi kutumia mbinu kadhaa ili kupata pesa za ada na sare kwa lengo la kurudi shule, lakini jitihada zake ziligonga mwamba.

Kwa kuirejelea nadharia ya Sosholojia katika msingi/ muhimili wake wa dhima kwa jamii unaoakisi uhusiano baina ya watu, inawataka jamii kuwa na mashirikiano miongoni mwao kwasababu suala la malezi ya watoto ni jukumu la kila mwanajamii na kuwafichua waovu katika jamii yetu kwani waswahili wanasema: Mbomoa nchi ni mwananchi.

### 4.6.3 Malezi ya Watoto kwa Vyombo vya Dola (Polisi)

Kama tulivyosema hapo awali kuwa, Serikali ndio chombo kikuu cha malezi ya watoto nchini. Pia zipo taasisi mbalimbali zinazojishuhulisha na malezi ya watoto, mfano: Mahakama, polisi, Vyuo vya mafunzo, Magereza na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto, n.k. Taasisi hizi miongoni mwa kazi zake ni kusimamia haki za msingi za watoto zinapatikana pasipo na shaka yoyote.

Pia watoto kama viumbe wengine kwa lengo la kuwajenga kuwa raia wema wa baadae, ni lazima wanapokosea ni jukumu la wazazi/walezi, jamii na serilkali kwa ujumla kuwasimamia watoto hao katika kuwaadabisha kwa lengo la kuwajengea misingi imara ya kimaisha. Hivyo serikali kwa upande wa watoto imeweka taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusimamia, kuzilinda na kuzitetea sheria zinazowahusu watoto hao kupitia vyombo kama Jeshi la polisi, Mahakama, Magereza n.k. Ni kawaida ya mtoto pale anapokengeuka malezi, taratibu au sheria za nchi kuonywa na kurekebishwa kwa lengo la kumkuza kiakili, kiroho na kumpa maadili yaliyotukuka.

Mtafiti kupitia mwandishi wa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* amebaini kuwa, Serikali, kupitia Jeshi la Polisi limechukua nafasi kubwa katika kumuadilisha na kumlea mtoto, hili limedhihirika kupitia watoto Musa, Peter na Kurwa kukamatwa na jeshi la polisi baada ya kubainika kuwa wanajishirikisha katika uuzaji wa madawa ya kulevya, jambo ambalo serikali inalipiga vita kwa sababu matumizi ya madawa ya kulevya ni kinyume cha sheria za nchi. Mwandishi amelidhihirisha hili kwa kusema:

> Mtu mwengine aligonga mlango nje na kabla hawajaitikia, polisi wawili waliupiga kumbo ule mlango, wakaingia.Walimsukuma Kurwa akaanguka chini. Mmoja wa polisi aliwaelekeza bastola wote watatu.
> "Mikono juu. Watoto wapumbavu! Majambazi wakubwa nyinyi!" "Nani Musa kati yenu?" "Mimi," Musa alijibu huku akitetemeka, tayari mkojo unamchuruzika.
> Kurwa aliinuka, akapokea amri, " Mikono juu! Na wewe ndiye mke wao! Basi leo mtajuta, mtajua jela ni nini. Mnauza dawa za kulevya badala ya kwenda shule!" Sasa aliwanasa makofi na kuwapiga mateke. (Uk 97)

Mtafiti amebaini kuwa huruma hailei mwana, jeshi la polisi imewaadilisha watoto hawa bila ya kuwaonea huruma baada ya kuwakamata chumbani kwa Musa na kuwakuta na paketi tatu za unga (madawa ya kulevya.) (uk.97).

Sambamba na hilo, ukosefu wa malezi bora kutoka kwa wazazi / walezi, taasisi za serikali (shule) kunakosababisha baadhi ya watoto kuwa nje ya mikono ya wazazi /walezi husababisha watoto kuwa waathirika wa mwanzo. Tendo linalowapelekea kuishia mikononi mwa vyombo vya dola au kufariki dunia. Kama tulivyoona kwa wahusika Dan, Kurwa, Musa, Peter na Zita.

### 4.6.4 Malezi ya Watoto Mitaani

Malezi ni mchakato ambao unajumuisha mtoto kupata chakula bora, elimu, matibabu, malazi n.k. Ni jukumu la mzazi kuhakikisha ustawi wa mtoto kupata malezi bora. Mtoto anapokosa familia, au mlezi huathirika kisaikolojia na hatimae kukosa muelekeo mwema wa maisha na kujiingiza katika matendo maovu. Serikali kwa ujmla wake inajukumu la kusimamia utekelezwaji wa haki zote zinazowahusu watoto.

Zipo sababu mbalimbali zinazopelekea watoto kuwa ni wa mitaani, miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na: kukosa haki za msingi mfano, chakula, malazi, mavazi, ulinzi, elimu, upendo, matibabu n.k, Wazazi kutengana, kufiwa na mzazi mmoja au wote wawili, kukosa mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ukiwemo upendo kutoka kwa wazazi, walezi kwa ujumla, kipato duni katika familia, migogoro katika ndoa n.k huwa ni miongoni mwa sababu zinazopelekea watoto kuwa wa mitaani. Mwandishi wa riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*, hakuwa nyuma katika kuibua dhamira ya malezi kwa kusema:

> Musa alikuwa karibu umri sawa na Peter .Wote walikuwa wamekumbwa na amri ya Mwalimu Mkuu, Chikoya. Musa, mtoto wa mwenye mama lakini hana baba, hakuwa na la kufanya …"Mama yako anasemaje?" "Aa! Mama ana hamsini zake. Na mimi nina sitini zangu," Musa alijibu.… Sasa Musa alitoa majani ya mirungi kutoka mfukoni. Aliyatazama kidogo, kisha akaanza kuyatafuna kama mbuzi. Peter alishangaa, " Musa ni juzi tu umeacha shule lakini ghafla umekuwa hivi?" Musa alicheka, " We Peter unachekesha. Sasa kwani nimebadilikaje? "Ee! na mirungi vilevile."Musa alisema, "Mimi nimeanza kula mirungi hata kabla sijafukuzwa shule. Fegi vilevile navuta." "Na mama yako?" "Ooho! Mama kinamuhusu nini yeye?" Musa alizidi kumshangaza mwenzake. (U.k.17-18.)

Mtafiti anaunga mkono msemo wa wahenga: "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Mama Musa hakuwa na nafasi ya malezi kwa mtoto wake jambo lilompelekea Musa kukosa malezi mema na hatimae kujiingiza katika matendo maovu kama vile utumiaji wa madawa ya kulevya, wizi na ujambazi.

Vile vile mwandishi amemchora Dan, mtoto mwenye umri wa miaka 12 ambae hakuwa na baba lakini akiishi na mama tu na kwa bahati mbaya hakumjali kimalezi. Mwandishi anasema:

> Saa 12 jioni Doto alirudi nyumbani. Hakuwa peke yake, alikuja na rafiki yake Dan wa miaka 12 hivi, aliyeishi Temeke. Hakuwa na baba ila mama ambaye hakujali kumlea, kumsomesha, wala kumlisha ipasavyo. Katika hali hii ngumu, Dan akajifunza mapema kuyakabili maisha kwa kujitegemea, hasa kwa njia ya uchokoraa, udokozi na wizi. Alipoingia kituo cha basi hakutoka mikono mitupu.Wasafiri wanawake ungewasikia wakilia machozi, "Aii! Yarabi pochi yangu! Nimeibiwa pesa zangu zote jamani!" Wakati huo aliyeibiwa akilia na kuchacharika, Dan, atakuwa zamani, kayoyoma. Alipoingia dukani, Dan bila Mhindi kujua, alitoka na saa, bangili, mkufu wa dhahabu ama chochote ambacho angekiuza, akapata pesa, akala, akashiba. Na alipopata pesa zaidi, basi Dan alimpitia rafiki yake Doto, wakaenda *Empire Cinema* kushuhudia bastola na masumbwi ya watemi wa Ulaya. (Uk.38 - 40)

Mtafiti amebaini kwamba,maendeleo ya sayansi na teknolojia yamechangia kumuathiri mtoto kimalezi kama mwandishi alivyoonesha matendo ya Dan kwenda sinema na kujifunza ujambazi. Uhuru wa kukosa malezi kunapelekea mtoto kuishi atakavyo mitaani na kurithi matendo maovu.

Pia Mbogo, katuchorea mtoto /watoto wanaoishi na mzazi mmoja na baadae kufariki kwa mzazi na mlezi wao, ambao ni Kurwa na Doto baada ya kufiwa na mama yao wakiwa wanaishi katika mazingira magumu, watoto hawa waliishia kuwa chokoraa na kutafuta riziki zao jalalani, mfano;

> “Mama yake Kurwa na Doto alikuwa mama wa hivihivi tu. Hivyo hakumjua baba wa watoto wake. Kabla hajajifungua watoto hawa mapacha, alijulikana kama Mwamvita. Alipokufa na kuwaacha wanawe wadogo, alijulikana kwa jina la Mama Kurwa. Siku ilipofika saa 8:02 usiku, Mama Kurwa alikata roho. Japo Jane, hakujaaliwa mtoto, sasa alikuwa na watoto! Ilibidi awalee watoto wa marehemu rafiki yake …Lakini wale pacha hawakuwa na bahati kwani Jane, mama yao wa kambo, alipatwa na ajali ya gari, akafa. Yalikuwa majonzi makubwa kwa Kurwa na Doto. Wakiwa na miaka minane tu, makucha ya dunia yaliwatazama bila huruma: njaa, malezi, maradhi na nini sijui! (36-37)

Hapana shaka yeyote mwandishi amedhihirisha tabia ya malezi na makuzi ya watoto wa mzazi/mlezi mmoja na kuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu imeonyesha dhamira ya malezi kwa watoto yalivyojitokeza kwa kutumiwa wahusika mbalimbali waliomo katika riwaya kama Kurwa na Doto, Dan na Musa ni watoto wa mitaani. Watoto hawa wamekuwa ni kielelezo na dira ya uhalisia wa maisha kwa jamii, kudhihirisha maisha halisi ndani ya jamii zetu yanayokabiliwa na umasikini, ulevi kwa baadhi ya wazazi, ukosefu wa elimu kwa watoto, uvivu , ukahaba n.k na kuishia watoto kuwa wa mitaani.

Mtafiti kupita nadharia ya Sosholojia inayorejelea mhimili wake wa dhima ya kijamii, amegundua kuwa, hali halisi ya jamii katika mila, desturi na mpangilio wa maisha husika wazazi/walezi wengi huathiriwa na umasikini ambapo hupelekea kuathirika kwa mila, utamaduni, maadili, malezi kwa watoto katika jamii na wazazi/walezi wengine kujiingiza katika matendo maovu ikiwemo uasharati na kupelekea kupatikana kwa watoto wa nje ya ndoa. Nadharia hii inawaasa wazazi, kuacha migogoro ndani ya ndoa zao ambayo huweza kupelekea kutengana kwa wanafamilia na kuachana na matendo machafu kama; ukahaba, kutupa au

kuwatelekeza watoto n.k badala yake wajitambue na wasiwe tayari kujiingiza katika maovu, wawe wabunifu na kushirikiana kuunda vikundi vya kimaendeleo na kuwa wajasiriamali n.k kwa lengo la kujinasua kiuchumi na kijamii kwa mustakabali watoto hao na taifa kwa ujumla.

Vilevile mtafiti amebaini kuwa ukosefu wa kuwakosa wazazi au mzazi hupelekea mtoto kuathirika kisaikolojia kama mwandishi alivyo mchora Kurwa kwa kujisemea peke yake kwa kumuuita mama na kujijibu mwenyewe. Mfano:

> Kurwa alifumba macho, moyo wake akatoka chozi. Nafsi yake ikamsimanga na kumuuliza, “Mama? Mama yuko wapi? Baba yuko wapi? Mapenzi yao yako wapi?” Vicheko na tabasamu zao zikowapi? Alikaa pale kwa muda…Kurwa aliwalaani mbwa wale kama vile wao ndio waliokuwa chanzo cha jitimai na tabu zake. (Uk.38)

Mwandishi anaonyesha kuwa Kurwa ameathirika kisaikolojia kwa kuwakosa wazazi wote wawili, hali iliyompelekea kuongea nafsini mwake akitamani kupata mtu wa kumuita mama. Watoto wananafasi yao ya kupata ushauri kutoka kwa wazazi pale inapobidi, lakini kwa upande wa mtoto Kurwa haikuwa hivyo bali imemfanya kuwa na upweke, kushindwa kutoa mawazo yake ambayo wakati mwengine yanagusa kile anachokipenda ambapo angepata nafasi angetumia kujieleza na kuonyesha kipaji chake kwa jamii. Mwandishi ameyathibitisha maelezo hayo kwa kusema:

> Kurwa alikuwa mwenye furaha. Maman’tilie mara moja aligundua kuwa mtoto yule alikuwa mwenye nguvu na bidii ya kazi. Mara kwa mara ungemsikia Kurwa akisema,”Mama acha hivyo vyombo, nitaviosha mimi,” au mama nipe nguo zako nikufulie” Au “Vipi mama?”Una homa? “Mama!...Mama!” “Mama …” Maishani hakuwahi kuujua utamu wa neno hili- Mama. Sasa aliupata utamu. Hivyo, akawania kuula, kuumeza ndani ya kifua na moyo wake mchanga. (Uk.76)

Mwandishi anaendelea kutuonyesha kuwa athari ya watoto wa mitaani huwapelekea watoto hao kukosa utamu wa kujua umuhimu wa mama na baba na familia kwa ujumla. Hivyo basi watoto wapewe nafasi ya kusoma na sio kufukuzwa shule kwa visingizio kadhaa , hii hupelekea taifa kujilimbikizia mzigo na kukosa nguvu kazi ya baadae.

## 4.7 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua kwa kina data za utafiti ambazo zimepelekea kukamilika kwa malengo ya utafiti. Madhumuni mahususi ya utafiti huu yamekamilika pamoja na maswali ya utafiti kujibiwa kama ilivyohitajika. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti ulifanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi ambapo katika lengo mahsusi la kwanza mtafiti amechambua mandhari, muundo,wahusika, na matumizi ya lugha zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Baada ya hapo mtafiti amechambua kwa uwazi dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tiliye* kupitia malezi ya baba na mama, malezi ya Majirani, malezi Shuleni, malezi ya Polisi na malezi ya mitaani. Hii inatoa ithibati kwamba, madhumuni mahsusi ya utafiti huu pamoja na maswali yake yamekamilika na kwa hiyo lengo kuu la utafiti nalo limekemilika. Katika sura ya tano itaangalia muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo mwisho katika utafiti huu, imetoa muhutasari, hitimisho na mapendekezo kuhusu utafiti mzima pamoja na matokeo yake. Sura hii imefupisha mambo mengi yaliyosemwa katika utafiti huu, kwa lengo la kumwezesha msomaji kupata picha ya utafiti mzima pale anaposoma sura hii na mwisho ni sehemu ya mapendekezo ya utafiti kwa ajili ya utafiti wa baadae.

## 5.2 Muhutasari

Utafiti huu umekamilika baada ya kutimizwa malengo mahsusi mawili ya utafiti ambayo ni: Kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*, na kuchambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Kukamilika kwa malengo haya mahususi kuliwezesha kujibiwa kwa maswali ya utafiti huu ambayo yalikuwa: Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya teule ya *Watoto wa Mama N'tilie*? Ni dhamira zipi za malezi ya watoto zilizojitokeza katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*?

### 5.2.1 Mbinu za kisanaa katika ujenzi wa Malezi ya Watoto

Utafiti huu umechunguza mbinu kadhaa za kisanaa katika ujenzi wa dhamira za malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* zikiwemo; mandhari, muundo, wahusika na lugha. Utafiti huu umebaini kuwa mwandishi ametumia

mandhari halisi ya maeneo ya jijini Dar-es-Salaam, kuwakilisha miji na vitongoji vyote nchini. Pamoja na hayo mtafiti kupitia mbinu ya muundo wa visa katika riwaya teule, mtafiti amebaini kuwa ni mtiririko wa namna ya kurukiana, kueleza kisa kimoja kabla ya kukimaliza anarukia kisa kingine, kwa upande wa wahusika mwandishi amefanikiwa kuwachora wahusika watoto kufikisha dhamira halisi ya malezi ya watoto kwa jamii za kimasikini nchini, tamathali za semi katika riwaya teule zilizowasilishwa ni tashibiha, tashihisi, sitiari na mbinu nyengine za kisanaa ambazo ni; takriri, tanakali sauti, nahau, methali, misemo na mbinu ya kitaharuki, hizi zilitumika katika kuibua dhamira ya malezi kwenye riwaya husika.

### 5.2.2 Dhamira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya Teule

Katika kuwasilisha dhamira za malezi ya watoto kwenye riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*, utafiti huu umebainisha, dhamira za malezi kwa familia (baba na mama), malezi ya watoto kwa majirani, malezi ya watoto shuleni, malezi ya watoto katika vyombo vya dola (polisi) na malezi ya watoto mitaani. Vipengele hivi vimebeba uhalisia katika maisha ya kila siku, kijamii na kitaifa nchini Tanzania, kutokana na maisha ya watanzania wengi masikini hukumbwa na kadhia hii katika malezi, umasikini na ukosefu wa huduma sahahi za afya.

## 5.3 Hitimisho

Kwa ujumla utafiti huu umefanikiwa kutimiza malengo yake mahususi ambayo yalikuwa mawili na kujibu maswali ya utafiti yaliyokuwa mawili. Lengo mahsusi la kwanza lilikuwa ni :

Kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie*. Matokeo ya utafiti wa lengo mahususi la kwanza yameonyesha kuwa, riwaya hii imetawaliwa na ubunifu wa mandhari mbalimbali katika kujenga mazingira halisi ya ujenzi wa malezi ya watoto. Uundwaji wa wahusika umegusa hisia za wasomaji katika kuibua dhamira ya malezi ya watoto pamoja na lugha iliyotawaliwa na tamathali za semi hususan tashibiha.

Lengo mahususi la pili lilikuwa ni kuchambua dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie.* Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa, riwaya hii imesawiri dhamira zilizomo za malezi kwa watoto ambapo wazazi (baba na mama), majirani, vyombo vya dola (polisi), shule, na mitaani lazima kuwepo kwa mawasiliano na mashirikiano katika suala la malezi mema ya watoto.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza fani na dhamira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* ya mwandishi E. Mbogo. Msanii huyu ameandika riwaya na tamthilia nyingi. Mtafiti anashauri kuwa, kupitia mada inayohusu watoto bado haijafanyiwa utafiti wa kutosha kupitia riwaya za Mbogo. Mwandishi katika kazi zake nyingi za tamthilia au riwaya, watoto ni sehemu ya wahusika wake. Mara nyingi watoto hao, hubeba ujumbe mzito kwa jamii na taifa. Ni budi watafiti wengineo kufanyia utafiti mada mbalimbali kama "Kuchunguza dhima za watoto katika kazi za E.Mbogo"au "Kuchunguza fani na dhamira za watoto katika kazi za fasihi."

## MAREJELEO

Adam, J. na Kamuzora, F (2008). *Research Methods for Business and Social Studies,* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar - BAKIZA (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha,* Nairobi: Oxford University Press.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*, Berkely: University of Califonia Press.

Buliba, A na wenzake (2014). *Misingi ya Nadharia na Utafiti,* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited

Cobley, P. (2001). *The Routledge Companion to Semiotics and Linguistics*, London: Routledge.

Cuddon, J. A. (1998). *Dictionary of Literary Terms and Literary Theory.* Great Britain: Andre Deutsch.

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary,* 7th ed. Oxford: Oxford University Press.

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Kezilahabi, E. (1983), "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi," katika, *Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3,* Dar es Salaam: TUKI, Kur. 226-243.

Khatibu, M.S. (1986), Tamathali za Semi za Kiswahili," katika *Mulika* namba 18, Dar es Salaam: Tuki, Kur. 1-15.

Kimambo, S. (2015). Kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za Kiswahili: Uchunguzi kifani wa riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Tasnifu ya M.A. Kswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa)

Kothari C. K. (1993) na (2008). *Research Methodology, Method and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kothari C. K. (2008) *Research Methodology. Method and Technique*. New Delh: New Age International (P) Limited.

Madumulah, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi,* Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mbogo, E. (2005). *Watoto wa Mama N'tilie,* Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.

Mjema, R. (1990). "*Kusadikika*," katika *Mulika* namba 22, Daer es Salaam: TUKI, Kur. 26-31.

Mlacha, S.A.K. na Madumulla, J.S (1991) *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msacky, E. (2015) Kuchunguza dhamira za Kijamii na Kisiasa katika riwaya ya *Siri za. Maisha.* Tasnifu ya M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Msokile, M (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EAEP Ltd.

Msokile, M. (1992).*Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor ltd.

Mulokozi, M. M. (1990), "Utunzi wa Riwaya ya Historia," katika *Mulika* namba 22, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-10.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*: *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Njogu na Chimerah (1999): *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa kazi za fasihi*, Augustana College: Rock Island.

Sengo, T. S. Y. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi,* Dar es Salaam: AERA.

Senkoro, F.E.M.K (1982) *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F.E.M.K., (2006), "Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Wamitila K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K.W.(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.